# Nipashe

Jumatatu Novemba 30, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580415

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Watumishi** TRA wakutwa na kesi ya kujibu tuhuma rushwa

UKURASA 3




**Ripoti:** Kigugumizi kinavyoweza kutibika

UKURASA 4




**'Pengo la Van Dijk halizibiki Liverpool'**

UKURASA 20

# Bashiru awakaribisha CCM wanawake 'majembe' upinzani



• **Awamwagia** sifa kwa kupambana Oktoba, ataka msako mamluki waliokihujumu chama... *Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**MENEJA FINCA, WENZAKE KORTINI TUHUMA ZA WIZI**

WAFANYAKAZI wanne wa Benki ya Finca Tawi la Geita, wamefikishwa...


# Lissu afunguka Viti Maalum CHADEMA

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wapili kushoto), alipowasili katika semina maalum iliyoandaliwa na Benki ya CRDB kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na taasisi mbalimbali za serikali na sekta binafsi kujadili fursa mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo, katika kufanikisha miradi ya maendeleo nchini. Kushoto ni Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Maulid. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




# Magufuli aanza uteuzi nafasi zake kumi

UKURASA 8


**MICHEZO** **KAZE NA UAMUZI MGUMU YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Lissu afunguka Viti Maalum CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amefunguka kuhusu uteuzi wa wabunge wa viti maalum ndani ya chama hicho.

Akihojiwa na televisheni moja kwa njia ya mtandao, Lissu, alisema, utaratibu wa upatikanaji wa wabunge hao ndani ya CHADEMA hufanywa na Baraza la Wanawake wa Chama hicho (BAWACHA), kuanzia ngazi za chini na mwisho humalizia kwa kupeleka majina matatu kwa Kamati Kuu kwa uteuzi.

"Utaratibu wa kuchagua viongozi ndani ya chama chetu huanzia kwa BAWACHA kuanzia ngazi ya chini majimboni, na mwisho wa siku kwenye Kamati Kuu ambako huwa wanatuletea majina matatu waliyoyapata kila mkoa, bila kujali nani wa kwanza na nani wa mwisho," alisema Lissu.

"Lakini cha kushangaza katika hawa 19 waliokwenda kuapa huko Dodoma ambao wengi ni viongozi wa juu wa BAWACHA akiwamo Halima Mdee (Mwenyekiti), Hawa Mwaifunga (Makamu Mwenyekiti), Grace Tendega (Katibu Mkuu), nani aliyeamua?" Alihoji Lissu.

Alisema anashangaa kilichomkumba Mdee kwa kuwa anafahamu utaratibu wote wa namna ambavyo wabunge wa viti maalum hupatikana.

"Halima Mdee ni miongoni mwa watu ambao naye alishawahi kuteuliwa na chama kuwa mbunge wa viti maalum na utaratibu wote anaufahamu, lakini cha kushangaza ni kitu gani kimemkumba wakati huu na kwenda kinyume na utaratibu wa chama," alihoji Lissu.

Kwa mujibu wa Lissu, mpaka sasa kwa siasa za Tanzania, wabunge wote wa viti maalum pamoja na kwamba huendesha uchaguzi wa kuchaguana wenyewe, lakini uamuzi wa mwisho huwa ni wa chama husika na si vinginevyo.

"Masuala ya nani awe mbunge wa viti maalum mpaka sasa kwa Tanzania, bado ni la Katiba ya vyama husika, na viti hivyo ni sehemu ya vyama ambalo mwisho wa siku vyenyewe ndio huamua," alisema.

"Namna pekee ya kiongozi wa kuchaguliwa ni kuwa mwanachama wa chama cha siasa aliyependekezwa na chama cha siasa, huo ndio utaratibu uliopo kwa sasa, hakuna namna nyingine. Huwezi kuwa mbunge kama hujapendekezwa na chama cha siasa."

"Walichokifanya hawa 19 waliokwenda kuapa wamekula njama ya kukisaliti chama, wakikimbilia wasizikose nafasi kinyume na taratibu za chama."

Kwa mujibu wa Lissu, CHADEMA ni miongoni mwa vyama ambavyo vilitoa fursa kubwa kwa wanawake hususani katika uchaguzi wa mwaka huu kwa kuwateua kugombea kwenye majimbo.

"Labda niwaeleze tu wale wanaosema CHADEMA ina mfumo dume. Chama chetu ndicho pekee ambacho kilitoa wanawake wengi kwenda kugombea ubunge kwenye majimbo kuliko chama kingine chochote, kati ya wagombea 244 kati ya hao 62 walikuwa wanawake, sasa mfumo dume unatoka wapi hapo," alihoji Lissu.



Mbunge wa Nachingwea, Dk. Amandus Chinguile, akichangia hoja kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Lindi, kilichokutana mwishoni mwa wiki mkoani humo. Kulia ni Mbunge wa Liwale, Zuberi Kuchauka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bashiru awakaribisha CCM wanawake 'majembe' upinzani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ali (pichani), amesema chama chake kinawakaribisha wanasiasa wanawake 'majembe' wa upinzani watakao hitaji kujiunga na chama hicho.

Dk. Bashiru aliyasema hayo jana jijini hapa, wakati alipokuwa akifungua semina ya siku mbili kwa sekretarieti ya CCM na kamati za utekelezaji za jumuiya tatu za chama hicho.

Alisema katika uchaguzi mkuu 2020, wanawake kutoka vyama vya upinzani pamoja na wa CCM, wameonyesha ushindani mkubwa wa kisiasa hali iliyoonyesha walivyo na uwezo mkubwa wa uongozi.

"Mwaka huu tumeona nguvu ya kinamama wa upinzani na hata ndani ya CCM, katika kupambana kwenye nafasi za ubunge haijalishi wapo katika chama kikubwa au kidogo cha siasa kutokana na hali hii napenda kuwaambia kinamama wa vyama vya upinzani majembe wenye uwezo karibuni CCM," alisema Dk. Bashiru.

Kadhalika, alisema kutokana na wanasiasa wanawake kuwagaragaza wagombea wa ubunge wanaume katika uchaguzi mkuu 2020, inamaanisha kuwa wana uwezo mkubwa ambao chama kinatakiwa kuutumia.

"Kama yule mbunge mwanamama wa CHADEMA aliyemshinda Kessy (Ally) kule Jimbo la Nkasi Kaskazini, pale kumtoa Kessy siyo jambo jepesi inatakiwa mtu mwenye uwezo, lakini pale Mbeya Mjini kwa Naibu Spika, hali hii inamaanisha kuwa kinamama wanastahili kupelekwa kwenye majimbo magumu ili kuyarejesha," alisema Dk. Bashiru.

Aliziagiza jumuiya za CCM kufanya uchunguzi na tathmini ya kina kubaini mamluki na maadui waliokihujumu chama wakati wa uchaguzi mkuu, Oktoba 28, mwaka huu.

Dk. Bashiru alisema uchaguzi huo umeweka historia ya aina yake katika demokrasia za vyama vingi nchini ambao umeonyesha dhahiri maadui wa nchi na marafiki wa kweli kupitia mijadala na hoja mbalimbali zilizoibuka.

Alisema ushindi uliopatikana ni matokeo ya uchapakazi wa jumuiya zote kupitia mabalozi wa CCM zaidi ya 250,000 ambao ndio wenyeviti wa mashina ya chama.

"Uchaguzi umetuonyesha marafiki wa kweli na maadui wa kweli, kumeibua mijadala na hoja nzito zenye viashiria vya chuki, mamluki na ukuwadi wa kisiasa hata hivyo Mwenyezi Mungu ametujaalia tumevuka salama," alisema.

"Tuendelee kufanya tathmini ya kina wapi tumefanya vizuri, nani ametuunga mkono, nani ametuhujumu, nani rafiki na adui wa kweli, hayo ni maagizo ya kamati kuu," alisisitiza Dk. Bashiru.

Pia, aliwaagiza wajumbe wa semina hiyo kuhakikisha kuwa wanapotoka katika mafunzo hayo wanaanza mara moja kuweka mipango ya kufanikisha uchaguzi ndani ya chama unaotarajiwa kufanyika 2022.

Alisema, pamoja na mambo mengine wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanahakiki wanachama na kusajili wengine ili kukiongezea nguvu chama.

Vile vile, alisema kuwa baada ya uchaguzi mkuu 2020, kupita na chama hicho kushinda kwa kishindo wanatakiwa kutobweteka bali wafanye kazi ya kuisimamia serikali ili kutekeleza ilani ya chama.

"Tuacheni mbwebwe za kuvaa 'green' lazima tuisimamie serikali hatutakiwi kuwa na mdahalo na kiongozi ambaye siyo mwadilifu kwani mwisho wa siku serikali haitafuti kura sisi wanaCCM ndiyo tunatafuta kura kwa wananchi," alisema.

Akizungumzia matokea ya uchaguzi mkuu 2020, ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na baadhi ya vyama vya upinzani kuwa CCM, iliiba kura alisema hiyo ni dhana potofu.

Alisema kuwa CCM haijaiba kura, bali watu waliotumika kukipa chama hicho ushindi ni mabalozi ambao ndiyo wamefanya kazi kubwa kusababisha waibuke kidedea.

"Kama wanatafuta mchawi wakaulize nyumba za mabalozi wetu, walijipanga kama nyuki, hawakujali tunapambana na mamluki, vyama dhaifu, vilivyo na sera dhaifu na vilivyogawanyika, Kamati Kuu imeelekeza sekretarieti kuhakikisha mabalozi wa CCM, wanaenziwa, wanaheshimiwa na kusikilizwa," alieleza.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Gaudensia Kabaka, alisema mafunzo hayo yatawajenga kuelekea uchaguzi ndani ya chama 2022 na uchaguzi mkuu 2025.

Hata hivyo, alisema kuwa hawatabweteka na matokeo ya uchaguzi mkuu 2020, waliyoyapata bali watafanya kazi kwa bidii ili kuendelea kuaminiwa na Watanzania kuendelea kuongoza serikali.





Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Dk. Bashiru Ally, akifungua kikao cha siku mbili cha Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM na Kamati za Utekelezaji za Jumuiya za Chama - UVCCM, UWT na Wazazi katika ukumbi wa White House jijini Dodoma. **PICHA: IKULU**

# Tanzania yatakiwa kuchukua hatua kuepusha kuwa jangwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

TANZANIA iko kwenye hatari kubwa ya kugeuka jangwa miaka 40 ijayo, iwapo wananchi wataendelea kuvuna kiholela misitu ya asili na kufanya shughuli za mbalimbali za kibinadamu bila kuzingatia matumizi endelevu hasa ya misitu ya hifadhi ya jamii.

Inaelezwa kuwa maelfu ya hekta zake hayajahifadhiwa kisheria.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Usimamizi wa Misitu Tanzania, MJUMITA, Rahma Njaidi, alisema hayo mjini Morogoro kwenye Mkutano Mkuu wa 20 wa mtandao huo uliokwenda sambamba na uchaguzi mkuu ambapo Revocatus Njau akachaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao huo.

Njaidi akashauri ili kukabiliana na hali hiyo, ni lazima misitu ya jamii ya vijijini ikatengwa na kurasimishwa kwenye ardhi ya vijiji, ambapo baadhi ya maeneo ikiwamo mikoa ya Morogoro na Lindi wamefanya hivyo na imeleta mafanikio makubwa.

Alisema iwapo misitu itatengwa na kurasimishwa, wananchi wataweza kushiriki kukihifadhi na kuvuna mazao ya misitu kwa maendeleo endelevu na kunufaika binafsi, kama vijiji na hata taifa kwa ujumla. "Wakiacha uvunaji holela, kuna hatari nchi kugeuka jangwa miaka 40 ijayo," alisisitiza Mkurugenzi huyo Mtendaji wa MJUMITA. Mkurugenzi Msaidizi wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania, TFCG, Emmanuel Lyimo, alibainisha kuwa utafiti uliofanywa na serikali kupitia Shirika la NAFOMA mwaka 2017, ulibaini hekta 469,000 zimekuwa zikipotea kila mwaka kutoka kwenye misitu isiyohifadhiwa kwenye vijiji.

Alisema ili kukabiliana na hali hiyo, ni vyema kuwa na usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii kwa kuzingatia wajibu wa jamii kuhakikisha wanasimamia misitu na kuwa na haki ya kupanga usimamizi wa misitu na mapato yatakayotokana na mazao ya misitu, ambapo kwa sasa asilimia 100 ya faida ya mapato hayo imekuwa ikienda kwa wananchi. "Wakiona wanafaidika watailinda misitu na kushiriki kuitunza na kuondoa hatari iliyopo ya kufanya nchi kuwa na ukame na hata kugeuka jangwa," alisema Lyimo.

Alifafanua kuwa katika takwimu za mwaka 2011, tayari kwenye vijiji 1,200 vilivyopangwa matumizi bora ya ardhi, ni hekta milioni mbili pekee za misitu ndio zimehifadhiwa, huku hekta milioni 22 bado kuhifadhiwa.

"Ndio maana tunawashauri MJUMITA msifanye kazi kwa mazoea, endeleeni kutumia sauti zenu kupiga kelele kwa wenye mamlaka, watunga sera na wafanya maamuzi kuwekeza kwenye kutunza misitu, itangazwe katika gazeti la Serikali na kukubalika kuwa misitu ya hifadhi ili misitu hiyo iwe salama.

Lyimo alisema misitu 51 imeshatangazwa kwenye gazeti la Serikali na kuhifadhiwa, ingawa bado kuna haja kutangaza misitu zaidi kwenye gazeti na kuhifadhiwa ili iwe salama zaidi.

Mwenyekiti wa Bodi ya MJUMITA, Revocatus Njau, alisema kutokana na taarifa yau tafiti ya NAFOMA ya 2015 inaonyesha Tanzania ina hekta milioni 48.1 ya misitu na kati yake, asilimia 46 ipo kwenye ardhi ya vijiji na haijahifadhiwa.

"Na katika suala la uhifadhi wa misitu ya vijiji, ni hekta milioni 1.8 tu ndio misitu iliyohifadhiwa ndio maana tunazidi kuhamasisha wanajamii, viongozi wa vijiji, watunga sera, watu wenye mamlaka kuhamasisha hii misitu ihifadhiwe," alisema.

# Watumishi TRA wakutwa na kesi ya kujibu madai rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, imewakuta wafanyakazi wawili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Geita wana kesi ya kujibu, baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wake.

Washtakiwa hao ni Sadick Lutenge na Elias Msule, ambao wanakabiliwa na makosa matano ya kuomba na kupokea rushwa chini ya kifungu cha 15(1)(a) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura 329 iliyorejewa mwaka 2019.

Uamuzi huo ndogo ulitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Obadia Bwegoge, baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wake na mahakama hiyo kuwaona washtakiwa wote wawili wana kesi ya kujibu kwa makosa yote matano.

Hakimu Bwegoge alisema upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi 10 na vielelezo 10, ambavyo vilithibitisha na kumfanya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo kutaka upande wa utetezi kutoa utetezi wake.

Washtakiwa wanatetewa na wakili wa kujitegemea, Liberatus John na upande wa Jamhuri ulikuwa ukiongozwa na mawakili wa serikali Agustino Mtaki na Kelvin Murusuri. Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili Murusuri alidai kuwa kosa la kwanza lilitendeka kati ya Mei 1 na Juni 4 mwaka 2019 Wilaya na Mkoa wa Geita, ambapo mshtakiwa Sadick Lutenge alishawishi na kuomba hongo ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Alphonce Miringo.

Murusuri alidai kuwa katika kosa la pili, mshtakiwa Sadick Lutenge alipokea rushwa ya Sh. milioni 10 kutoka kwa Alphonce Miringo.

Aliendelea kudai kuwa kosa la tatu lilitendeka kati ya Februari 1 na Aprili 8 mwaka 2019 Wilaya na Mkoa wa Geita, ambapo washtakiwa Sadick Lutenge na Elias Musula walishawishi na kuomba hongo ya Sh. milioni 75 kutoka kwa Bertha Magandula na Makoye Shinga kwa lengo la kuwafanyia makadirio ya chini ya hesabu za kodi walizotakiwa kulipa serikali.

Alidai kuwa kosa la nne lilitendeka kati ya Aprili 8 na 9 mkoani humo, ambapo washtakiwa wote Sadick Lutenge na Elias Msula walipokea hongo ya Sh. milioni 50 kama sehemu ya fedha iliyokuwa imeombwa ya Sh. milioni 75 kutoka kwa Bertha Magandula na Makoye Shinga.

Kadhalika, alidai kuwa kosa la tano lilitendeka Juni 14 mwaka jana Wilaya na Mkoa wa Geita, ambapo mshtakiwa Sadick Lutenge alipokea Sh. milioni 10 kama sehemu ya fedha iliyokuwa imeombwa Sh. milioni 30 kutoka kwa Alphonce Miringo.


## KUFUNGWA KWA KAMPUNI

**IJAMU COMPANY LIMITED**
**NAMBA YA KAMPUNI : 5982**

Kufuatia maamuzi ya Bodi ya wakurugenzi na wanahisa wa IJAMU CO.LTD imeamuru kufunga shughuli zake za biashara kuanzia tarehe 30/10/2020.

watu wote ambao wanaidai IJAMU CO.LTD wapeleke madai yao ndani ya siku 90 kuanzia tarehe ya tangazo hili katika ofisi za IJAMU CO.LTD

**Kwa mawasiliano**
**Mkurugenzi: IDDI JACKSON MULENGA (0754-595808)**
**SAIDI IDDI MULENGA (0768-078570)**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHINA RAILWAY MAJOR BRIDGE ENGINEERING GROUP CO LTD** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **WHEEL LOADAR** yenye namba za usajili **T542 CDQ CHASIS NAMBA ZL50CNL1207268,ENGINE NAMBA CL329318** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa:**
**DAR/ OST/RB/825312/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LABAN RUBANGO ANDREW** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **KLUGER STATION WAGON** RANGI NYEUSI YENYE USAJILI **T599DTC** CHASSIS NAMBA **ACU200058320** ENGINE NAMBA **2AZ0259453** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLIS KILICHO KARIBU.

**TAARIFA YA POLISI**
**MWA/NY/RB/826131/2020**

RIPOTI MAALUM

# Kigugumizi kinavyoweza kutibika

## ■Mtu anaweza kukipata ukubwani

Na Christina Mwakangale

UKIWA na kigugumizi pengine unaweza ukakosa hata ajira au mchumba. Kuna siku ilinichukua sekunde 60 kumaliza kutamka sentensi moja," ni maneno ya mwathirika wa tatizo hilo, Ally Abdallah.

Binadamu huzaliwa na hali hiyo ambayo ina vikwazo mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Kigugumizi, Oktoba 22, kila mwaka, waathirika wa tatizo hilo wanasema kuwa mtu akiwa na hali hiyo anakutana na vikwazo vingi.

Neno kigugumizi linatokana na kitenzi 'kugugumia' kwa Kiingereza 'stuttering' maana yake ni shida kwa baadhi ya watu wakati wa kusema au kutamka maneno.

Bingwa wa Masikio, Pua na Koo, kitengo cha Matamshi na Lugha, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Rachel Mkumbo, anasema tatizo hilo huwaathiri zaidi watoto wa kiume kuliko wa kike, na hasa walio kwenye umri wa kuanza kuongea wa miaka miwili hadi sita.




Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Mtindo Maalum wa Uzungumzaji Tanzania (CHAMMUTA), Ally Abdallah (katikati) akifanya mahojiano na mwandishi wa makala hii, kushoto kwake, Dudley Mbowe, mwanachama wa chama hicho.

### ALIVYOPATA KIGUGUMIZI

Ally Abdallah ni mwanazuoni na Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Mitindo Maalum ya Uzungumzaji Tanzania (CHAMMUTA).

Anasema aliamua kuanzisha chama hicho ili kutoa elimu kwa jamii kuhusu kigugumizi na kuondokana na unyanyapaa, dhana na imani potofu kwamba wenye tatizo hilo wana matatizo ya afya ya akili.

"Kwa bahati mbaya tupo kwenye dunia ambayo haina subira. Dunia inakwenda kasi, watu wenye kigugumizi tuna mazingira magumu sana, unazungumza na mtu ambaye hana subira hawataki kutuacha tumalize kuzungumza wanatukatisha," anabainisha Ally.

Iliwahi kunikuta kwenye usaili nilipata kigugumizi, jambo ambalo linaweza kuwa sababu ya walio na kigugumzi kukosa ajira katika baadhi ya maeneo.

Anasema baada ya kuhitimu masomo ya chuo, na kuamua kuanzisha chama hicho mwaka jana, ambacho kina wanachama 25, kinajumuisha wazazi na walezi wenye watoto walio na kigugumizi, baada ya kubaini huathiriwa zaidi.

"Nilipata kigugumizi nilipokuwa na miaka mitano, baada ya kufiwa na baba yangu mzazi, mama yangu alinielezea. Nilikuwa katika chumba alichokuwa amelazwa baba yangu na kushuhudia akikata roho," anasimulia Ally.

Kuna siku ilipita zaidi ya dakika moja bila kumaliza sentensi, ndipo nikaanza kutembea na kalamu muda wote na kuiweka pembeni ya sikio, ili nikihesabu sekunde kadha najua siyo hali ya kawaida, naamua kumwandikia ujumbe mtu kwenye karatasi badala ya kuzungumza.

Pamoja na kuwa na hali hiyo mama yake alikuwa na matarajio makubwa kutokana na kuwa ni mzaliwa wa kwanza kwenye familia ya baba ya watoto 15.

Anasema kuna wakati mama yake alitamani awe mzungumzaji mzuri na mtiririko mzuri kama vile Bill Clinton, rais wa zamani wa Marekani.

"Kuna wakati tulikuwa tunaangalia televisheni na mama, chaneli ya CNN, kipindi hicho Bill Clinton ni Rais wa Marekani, kama unavyojua Clinton alikuwa na 'flow' nzuri akitoa hotuba zake.

Mama aliniangalia akasema mwanangu huwezi kuwa kama Clinton. Nilimtazama sikumjibu, ila niliwaza huyu mama anawezaje kufikiri mimi kuwa kama rais wa Marekani na kigugumizi hiki."

Ally alijipa moyo kuwa mama yake hajui kuwa yeye ni Bill Clinton akiwa darasani.

Tangu akiwa shuleni hakutaka kuwaonyesha walimu wala wanafunzi kuwa ana tatizo la kigugumizi jambo lililomfanya kujipanga kabla ya kuanza kuzungumza.

Aliificha hali yake hiyo, lakini wakati anamaliza shule alipewa muda azungumze.

"Hapo ndipo nilijulikana ila sikutaka kujificha tena, niliona nitakuwa siwatendei haki walio na hali kama yangu. Nilipopewa muda wa kuzungumza na kurudi nyumbani, nikamweleza mama yangu, alishangaa."

Niliona bora hali ijulikane ili jamii ifahamu hali zetu," anabainisha Ally.

### ANAYOPITIA

Anasema pamoja na kuishi na hali hiyo kwa miongo kadhaa, hupatwa na hali ambayo haizoeleki.

"Ninapokuwa nimebanwa sana na kigugumizi huwa nakosa pumzi, ninapomaliza kuongea utaniona ninavyokuwa nimechoka, pumzi inakuwa imeisha."

Tangu apate kigugumizi uzoefu wake shuleni hadi chuo kikuu na kulingana na utafiti mbalimbali aliousomea na kufanya uchunguzi wake binafsi, amebaini mambo kadhaa.

### ALIYOBAINI

Anasema amebaini kuwa kuna masuala ya imani potofu, kunyanyapaliwa, tiba duni, na kufanya watu wenye tatizo hilo kuwa wapweke kulingana na jamii inavyowachukulia. Mara nyingi kigugumizi kinarithiwa iwapo mmoja katika familia anacho.

Anasema baadhi ya utafiti, unaeleza kuna watoto ambao wanaiga kigugumizi kutoka kwa mzungumzaji, hasa kutokana na tabia ya kuiga kila kitu.

Mzazi au mlezi anapaswa kumtazama machoni mtoto na kumwongelesha haraka haraka ili kuacha kuiga.

Anasema utafiti mwingine unabainisha kuwa kuna kasoro ya 'neurolojia' (mfumo neva unaojumuisha uti wa mgongo, ubongo na mishipa ya fahamu) inayoweza kuwa sababu ya kigugumizi ambayo mhusika amezaliwa nayo au kupata mshtuko.

"Sehemu hii inaweza kuwa kweli, kwa mfano mimi baada ya baba kufariki, wiki chache mama aliona nimeanza kupata kigugumizi, yawezekana nilipata mshtuko," anasema.

"Kwanza nilichelewa kuanza kuongea, niliongea nikiwa na miaka mitatu na nusu, baada hapo nilipofika miaka mitano kigugumizi kikaanza," anabainisha.

### UZOEFU

Ally anasema mtu mwenye kigugumizi unapoongea naye ni lazima umwangalie usoni ili aweze kujenga kujiamini.

"Ishara ni kwamba wakati tunazungumza ulikuwa unaniangalia machoni ukaacha kuniangalia sababu nimekwama kumalizia sentensi, ndio unanimaliza kabisa, cha msingi ni kuendeleza mawasiliano," anasema.

Anasema, kuna siku alikuwa anazungumza na mtu, kigugumizi kikamshika kwa muda wa sekunde 60, inavyoonekana mtu huyo alikuwa na haraka na kufanya kitu ambacho hatakisahau... "Alitoa mkono wake na kuangalia saa yake, muda wote huo bado nimeshikwa na kigugumizi, ilipita muda sijamaliza neno, kitendo cha kuangalia saa nilijihisi namchelewesha, lakini si kwamba nilipenda. Watu wenye kigugumizi tunahitaji subira."

Anasema jamii inahitaji kujengwa, kuelimishwa na kuwa na tabia ya kuwa na ustahimilivu kwa watu wenye kigugumizi.

### MAAJABU

Mtu mwenye kigugumizi akifuata 'melody' (mpangilio wa sauti) ya muziki, kigugumizi hupotea.

Katika njia ambazo nazitumia kupunguza kigugumizi ni kutumia 'tune' (mdundo) inapunguza sana, na herufi inayonipa shida sana kutamka ni 'A' na kibaya zaidi majina yangu yanaanzia na 'A'.

Najitahidi ninapojitambulisha sianzi na 'A', huwa nasema jina langu ninaitwa...fulani fulani."

### DAKIKA 20 ZA WASILISHO

Dudley ni mwanachama wa CHAMMUTA, anasema alipata kigugumizi akiwa na miaka minane na sasa umri wake ni miaka 28.

Katika maisha yake tatizo kubwa alilolipata akiwa shuleni na kutaniwa. "Wanafunzi wenzangu katika darasa moja na mimi walinitania, lakini niliishi hivyo hivyo nikamaliza sekondari nikaenda chuo."

Kigugumizi changu kina mtiririko na mara nyingine kinapotea kabisa na sababu sizijui nakumbuka kuna kipindi nikiwa kazini nilikuwa nafanya wasilisho ambalo bosi wangu alitakiwa alifanye, lakini alipata dharura.

Kitu cha dakika tano kilinichukua dakika 20, mtu ukiwa unafanya wasilisho wanaokusikiliza wanajua ni la muda fulani dakika tano au 10, ukitumia muda mwingi inawachosha.

Kigugumizi changu kilifanya niendelee kwa muda mrefu nikaona nawapotezea muda.

Anasema mama yake ana kigugumizi kidogo, sio kama chake ambacho anaona ni kikali zaidi na aliwahi kuongea akiwa mtoto kama watoto wengine, lakini alipotimiza miaka minane akaanza kushindwa kuongea moja kwa moja.

Hutumia mbinu mbalimbali ili kukiepuka kwa kutamka maneno tofauti ambayo yanamkwamisha.

"Ukiwa na kigugumizi watu wakakuambia vibaya muda mwingine utaona ni bora nisiongee na kuwa kimya, hii inakufanya uwe mkimya na kujitenga," anafafanua Dudley.

### YANAYOWAKWAZA

Ally anasema pamoja na kuikubali hali hiyo yapo mambo kwenye jamii na kwamba baadhi hudhani wenye kigugumizi ni wahalifu na wasahaulifu wa mambo, kutokana na tatizo lao.

Anasema changamoto kubwa inayowakumba ni pale mtu anapoamua kumalizia sentensi yake.

"Utakuna mara nyingi unapomuona mtu mwenye kigugumizi akikwama sentensi ni kama amesahau, sikweli, utakuta mtu anakumalizia sentensi.

"Hili suala linatukera, linavunja moyo, niache nimalize kuzungumza, si kwamba nimemaliza na unaweza kufikiria nataka niseme hivi kumbe sivyo, jamii isitusemee," anasema Ally na kuongeza.

"Unaponisemea kigugumizi huwa kinaongezeka zaidi unakuwa umenitoa kwenye mstari, pale mtu anapokusemea au kukuwekea maoni yake," anasisitiza.

Anasema msikilizaji hutakiwa kumpa subira mwenye kigugumizi, na haichukui sekunde tatu hadi 30 ili kumalizia sentensi moja.

"Utakuta mtu anakwambia polepole zungumza, usiwe na haraka, najiona kumbe sipo sawa, kigugumizi ndio kitachanganya."

Pia, anasema baadhi ya maneno yanayotumiwa na vyombo vya habari, hujiona wao ni sehemu ya tatizo kwenye jamii.

"Utakuta kichwa cha habari kinasema 'Mkurugenzi apata kigugumizi akihojiwa...hii sentensi nikiiona mimi niliye na kigugumizi nafikiria kwamba kigugumizi ni tatizo, watu waongo, wasio waaminifu," anabainisha."Au msanii anaimba 'nilipata na kigugumizi nilipokutana na mtoto mkali...' ni tatizo kwetu."

Anasema alipobaini neno kigugumizi jamii inalichukulia kwa mtazamo hasi, wakati wanaunda CHAMMUT, alifikiria kutotumia neno 'Chama cha wenye Kigugumizi' na badala yake kutumia mtindo maalum wa kuzungumza ili kubadili mtazamo.

**Itaendelea kesho**

HABARI KITAIFA

# Mwanafunzi abuni mfumo malipo kadri unavyotumia

**Na Mwandishi Wetu**

MWANAFUNZI wa Chuo cha Uhandisi na Teknolojia cha Al-Maktoum (AMCET) Dar es Salaam, amebuni mfumo wa kulipa maji kadri unavyotumia (pre-paid water system), ambao upo katika hatua za majaribio kabla ya kuanza kutumika rasmi na wateja.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya saba ya chuo hicho, Mwenyekiti wa Bodi wa Al-Maktoum, Prof. Hamisi Omar Dihenga, alisema mfumo huo umeshawasilishwa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa majaribio zaidi.

Dihenga alisema mwanafunzi huyo, Wilbroad Nyirenda, ni miongoni mwa wahitimu wa mwaka wa stashahada, na alikuwa ni mshindi wa tatu kitaifa wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) yaliyofanyika Machi mwaka huu na kukipa chuo heshima kubwa.

Alisema kwamba utasaidia sana wananchi kwenye matumizi ya maji na mamlaka za maji katika ukusanyaji wa mapato.

"Ukishaanza kutumika rasmi utasaidia kwa namna nyingi sana, tutafika sehemu tutakuwa tunaweza kupanga matumizi ya maji kwa umakini na mamlaka za maji pamoja na serikali kwa ujumla itakusanya mapato kwa usahihi," alisema.

AMCET ilianza kutoa masomo rasmi mwaka 2010/2011 na kinatoa astashahada na stashahadi katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia na kinadhaminiwa na Al-Maktoum Foundation Tanzania ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Mgeni rasmi kwenye mahafali hiyo, Balozi wa UAE nchini, Khalifa Abdulrahman Mohamed Al Marzouqi, aliwaasihi wahitimu watambue kwamba mafanikio yao ni miongoni mwa ishara za mafanikio ya chuo katika kuunga mkono jitihada za serikali kuleta maendeleo nchini.

Aidha, aliwashauri pia wazingatie maadili waliofundishwa chuoni hapo popote watakapoenda kutumikia taifa na wawe mfano wa kuigwa.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Hamdun Sulayman, alisema changamoto kubwa ya chuo hicho ni idadi ndogo ya udahili itakonayo na wanafunzi wengi wanaohitimu kidato cha nne kufeli somo la Hisabati, ambalo ni somo mama katika mafunzo ya uhandisi.




Mwenyekiti wa Baraza la Vijana (BAVICHA), Jimbo la Shinyanga Mjini, Samsoni Ng'wagi, akizungumza na waandishi wa habari kwenye ofisi za CHADEMA Kanda ya Serengeti jana, na kuwataka Halima Mdee pamoja na wenzake 18, watii maagizo ya chama hicho kwa kuomba radhi ama kukata rufani, baada ya kuvuliwa nyadhifa zao pamoja na uanachama. Kushoto ni Mwenyekiti wa BAWACHA Jimbo la Shinyanga Mjini, Zena Gulam, kulia ni Katibu Mwenezi, Ibrahim Isack. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Serikali yaelekeza nguvu kwenye sekta ya misitu

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imeanza kuboresha mazingira katika sekta ya misitu ili kuhakikisha inachangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi, kuwaongezea wananchi kipato na kuzalisha ajira.

Naibu Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Mohamed Kilongo, alisema hatua hiyo inalenga kuimarisha utekelezaji wa mpango wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ili shughuli za uchumi na biashara ziongezeke na kuzalisha ajira.

Alisema kama ilivyo kwa sekta nyingine, wanaamini kuwa sekta ya misitu ikiboreshwa zaidi na kuthaminiwa na wafanyabiashara, itakuwa ni mkombozi kwa Watanzania wengi.

"Miaka ya nyuma serikali ilianzisha mashamba makubwa ya mitiki ili kuepukana na matumizi makubwa ya mbao ngumu za miti ya asili, na ndiyo maana kwa sasa tumeona kuendeleza nia njema hiyo kwa kuweka mazingira mazuri zaidi katika kuhamasisha matumizi ya miti mingine ikiwamo ya misaji ambayo nayo ina ubora sawa na mbao za mninga na mkongo," alisema na kuendelea:

"TFS ina mashamba makubwa ya miti ya misaji ambayo kwa mwaka inatoa zaidi ya mita za ujazo 20,000 na tumeanza kuhamasisha watu watumie mbao za miti hiyo, lakini kuhakikisha mbao zake zinaingia kwenye mlolongo wa serikali na kutambulika kama ilivyo kwa mkongo na mninga."

Pantaleo Banzi, Mwenyekiti wa wafanyabiashara za samani wa Keko jijini Dar es Salaam, alisema wamebaini kwamba mbao za misaji licha ya ubora wake zinapatikana kwa urahisi na hivyo kuwashauri watu kuziangalia kwa jicho la tatu.

Mwakilishi wa wafanyabiashara wanaosafirisha mbao za misaji nje ya nchi, Malima Mrungu, alisema aina hiyo ya mbao imekuwa na soko kubwa na inapendwa zaidi nje ya Tanzania.

# Mkuu wa JKT ahimiza kuendeleza miradi

**Na Hellen Mwango**

MKUU wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Charles Mbuge, amewaasa maofisa na askari wa Kamandi ya Jeshi la Anga Ngerengere kuondoa ubinafsi na kushirikiana katika kulinda na kuendeleza biashara ikiwamo miradi ya kukuza uchumi, ili kuchangia pato la taifa kupitia ulipaji kodi.

Alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki katika ziara yake ya kikazi katika Kamandi ya Ngerengere ikiwamo kutembelea uwanja wa ndege pamoja na kufungua mradi wa bwalo la Ubena Resort unaotoa huduma kwa maofisa, askari pamoja na wananchi wanaozunguka eneo hilo.

"Sisi kama maofisa wakuu na wadogo pamoja na askari tuondoe ubinafsi, tushirikiane katika kuendesha huu mradi unaotuunganisha na wananchi wanaozunguka itaongeza ukaribu kwa wananchi na jeshi lao la ulinzi," alisema na kuongeza:

"Ninaamini tutachangia uchumi wa nchi kwa kulipa kodi kupitia mradi huu, Suma JKT inachangia Sh. milioni 10 taslimu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa nyumba ya kulala wageni ndani ya eneo la bwalo hili, pia nimeagiza Suma kununua mashine ya kufyeka nyasi katika uwanja wa ndege yenye thamani ya Sh. milioni nane badala ya kufyeka kwa mikono."

Akisisitiza kuhusu nidhamu kwa wanajeshi, alisema serikali ilitoa agizo kwa vikosi vyote kuwa na miradi mbalimbali kwa ajili ya kujiongezea kipato na kupata fedha za kujikimu kwa hiyo badala ya kwenda kupata huduma uraiani wapende vya kwao.

Alisema mbali na fedha za kuanza ujenzi wa nyumba ya kulala wageni, pia ameagiza Suma JKT kuwasilisha kreti 100 za bia na yeye atachangia 50 za soda katika kuinua mtaji wa bwalo hilo.

Alisema Suma JKT iko kwa ajili ya Jeshi na kwamba Sh. milioni 10 alizokabidhi zianze ujenzi mara moja wa nyumba ya kulala wageni waweze kuongeza kipato cha kujikimu.

Meja Jenerali Mbuge alikubali kuwa mshauri na mlezi katika mradi huo kwa kamandi hiyo, pia aliagiza mtaalamu kutoka Suma JKT kwenda kuzungukia eneo hilo mara moja ili waanze ujenzi.

Awali, Mkuu wa Kikosi cha 601, Kanali Zeno Sikukuu, alisema lengo kubwa ni kuboresha huduma za jamii katika eneo linalozunguka bwalo hilo, ikiwamo kuwa na nyumba ya kulala wageni ya kisasa, huduma za kijamii, mashine za kutoa fedha (ATM), maduka ya dawa na mahitaji yote ya kijamii.

Pia alisema wana lengo la kutengeneza maegesho ya magari ya kisasa.

"Afande Mkuu wa JKT, tunaomba ukubali kuwa mshauri wetu wa karibu na kuwa mlezi wetu katika mradi huu," alisema Kanali Sikukuu.

Naye Mkuu wa Shule ya Anga (SAK), Brigedia Jenerali, Wema Senzia, alisema wana matumaini makubwa ya kufanikisha mradi huo kwa kuzingatia ushauri na kuzingatia maagizo ya mkuu wao.

Mwasisi wa pili wa bwalo hilo, Mwambata wa Kijeshi nchini Ethiopia, Brigedia Mohamed Mohamed, alisema alipohamishiwa kikazi mapema mwaka huu aliona fursa ya kulifufua bwalo hilo, ili kutoa huduma kwa maofisa na askari wanapohitaji kujadili mambo mbalimbali ya kikazi na kijamii.

Kamandi ya Ngerengere inajumuisha vikosi viwili vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Kikosi cha 601 na SAK.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuzisapoti Simba SC, Namungu kimataifa

**WAWAKILISHI** wa Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa Namungo FC na Simba, mwishoni mwa wiki walishuka dimbani kuanza kupeperusha bendera ya nchini kwenye michuano ya Afrika kwa ngazi ya klabu inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani humu (CAF), Kombe la Shirikisho na Ligi ya Mabingwa.

Namungo inayopeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, Jumamosi ilianzia nyumbani katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Al Rabita ya Sudan Kusini.

Matokeo hayo yanaifanya, Namungo kuhitaji sare yoyote, ushindi ama kutopoteza kwa zaidi ya mabao 2-0 katika mechi ya marudiano itakayopigwa kati ya Desemba 4-6, mwaka huu nchini Sudan Kusini, ili kusonga mbele katika hatua inayofuata.

Hata hivyo, huenda Namungo ikazidi kufaidika kwa kupata nafasi ya kucheza mechi zote mbili hapa nchini endapo tetesi za Wasudan Kusini hao za kutaka michezo yote miwili ichezwe Tanzania kutokana na kutokuwa na uwanja unaokidhi viwango vya CAF, zitakuwa kweli. Na kwa upande wa Simba ambayo jana ilianzia ugenini nchini Nigeria katika mechi yao ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikicheza dhidi ya Plateau United kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa New Jos uliopo mji wa Jos umbali wa Kilometa 181 kutoka mjini Abuja, nayo itakuwa na kibarua kigumu Jumapili kuhakikisha inapata ushindi wa jumla ili kuwatoa Wanaigeria hao na kusonga mbele.

Tunatambua kwa wawakilishi hao wa Tanzania, wanahitaji kupata matokeo ya jumla, ili kusonga mbele katika michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika, hivyo njia pekee ni kuendelea kuzipa sapoti kubwa ndani na nje ya uwanja.

Bahati kubwa kwa wawakilishi hao wa Tanzania, wameruhusiwa na CAF mechi zao kuhudhuriwa na mashabiki asilimia 50 ya uwezo wa uwanja kutokana na Tanzania kutokuwa na hatari kubwa ya maambukizo ya virusi vya corona kama ilivyo kwa mataifa mengine kwenye michuano hiyo.

Mfano ni mechi hiyo ya Simba dhidi ya Plateau United nchini Nigeria haikuhudhuriwa na mashabiki kutokana na hatari kubwa ya maambukizo ya virusi vya corona vinavyoendelea kuitesa nchi hiyo ya Afrika Magharibi.

Lakini tunatambua kumekuwa na mgawanyiko mkubwa wa kiitikadi linapokuja suala la Simba na Yanga, kwa mashabiki wa soka kugawanyika na kushangilia timu kutoka nje jambo ambalo hupunguza hamasa kwa mwenyeji kushindwa kufaidika ipasavyo na mchezaji wa 12 ambaye siku zote huwa ni mashabiki.

Kwa ujumla, Nipashe tunakerwa na hatufurahii hata kidogo kuona Watanzania wakigawanyika kwa upande mmoja kutoa sapoti kwa timu za kigeni, hivyo mbali na kukemea tabia hiyo, lakini pia tunawasihi kuonyesha umoja wetu ili kuinua kiwango cha soka nchini.

Kama ilivyo rahisi kwa mashabiki wa Simba na Yanga kuungana kuipa sapoti timu kama Namungo ama zinginezo zinapoiwakilisha nchini kwenye michuano ya kimataifa, tunatamani kuona hilo likitokea msimu huu kwa mashabiki wa hao kuungana na kuwa kitu kimoja kuwasapoti wawakilishi hao wa nchi.

Tumelazimika kutoa rai hiyo hasa tukizingatia misimu miwili iliyopita kitendo cha Simba kufika hatua ya makundi kiliiongezea Tanzania pointi CAF na kuifanya msimu uliopita kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya Afrika, mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho.

Hatua hiyo ilitoa fursa kwa Yanga ambayo ilipoteza sifa ya kushiriki michuano hiyo kwa msimu uliopita, kukata tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo mafanikio ya timu moja inatoa faida kwa taifa kwa ujumla, jambo ambalo linaonyesha ni kwa namna gani mashabiki wa soka wanapaswa kuungana kuhakikisha wawakilishi wa nchi wanasonga mbele.

Nipashe tunawatakia kila la kheri wawakilishi wetu katika michuano hiyo, na daima tutaendelea kuhamasisha mashabiki kuwa kitu kimoja kwa faida ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hongera Namungo kwa ushindi, lakini timu bado

Na Adam Fungamwango

**KWA** mara ya kwanza kwenye historia ya Namungo FC, imecheza mechi ya kimataifa na kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Al Rabita ya Sudan Kusini.

Namungo, timu kutoka Ruangwa mkoani Lindi, Jumamosi iliyopita ilitengeneza rekodi yake safi, iliposhinda idadi hiyo ya mabao kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Timu hiyo iliyopanda daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu uliopita, ilipata mabao yake kupitia kwa Mgana Steven Sey ambaye alisajiliwa msimu huu akitokea Singida United iliyoshuka daraja.

Sey aliingiza Namungo kwenye rekodi dakika ya 20 kwa kufunga bao la kwanza kwenye michuano hiyo hatua za awali na 39, huku mchezaji wa zamani wa Simba, Shiza Kichuya akifunga ukurasa kwa bao la dakika ya 64.

Ni ushindi ambao unawapeleka Namungo hatua moja zaidi kuelekea raundi ya kwanza ya michuano hiyo, ambapo baada ya hapo itakwenda kwenye hatua ya pili kama itashinda na baadaye kucheza na timu ambazo zitakuwa zimetolewa kwenye raundi ya kwanza ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kabla ya kutinga hatua ya makundi.

Ni safari ndefu bado, lakini kama viongozi, wachezaji na benchi la ufundi litajipanga wanaweza kufika huko.

Kuna taarifa za ndani kuwa Al Rabita kutaka mechi yao ya marudiano ichezwe hapa hapa Tanzania, kutokana na uwanja nchini kwao kutokidhi vigezo vya Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Kama ndivyo, basi itakuwa ni faraja kwa Namungo na Watanzania kwa ujumla.

Nitoe pongezi kwa wananchi wote wa mkoani Lindi, viongozi na wachezaji wa timu hiyo kutokana na ushindi ambao umewapa faraja Watanzania wote.

Hata hivyo, kwa jinsi nilivyoiangalia mechi hiyo ni kwamba Namungo bado kuna maeneo inabidi ijirekebishe ili kuweza kupambana na timu ngumu itakazocheza nazo mbele ya safari.Kwanza kabisa kwenye mechi hiyo, Namungo ilikuwa na uwezo wa kushinda kwa mabao kuanzia matano na kuendelea. Ilikuwa ni mechi rahisi mno kuliko inazocheza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ukweli ni kwamba ilikutana na timu dhaifu, isiyokuwa na uzoefu na yenye wachezaji wa kawaida sana.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Morocco na viongozi wa Namungo wanatakiwa kipindi cha dirisha dogo waingie sokoni na kusajili wachezaji ambao wataweza kupambana na timu ngumu ambazo itakwenda kucheza nazo mbele ya safari.

Viongozi na wachezaji wa timu hiyo watambue kuwa kuna timu kubwa, ngumu, maarufu na zenye uwezo mkubwa huwa zinatolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na kuangukia Kombe la Shirikisho, hapo ndipo patakapoanza kuchimbika.

Unaweza kukutana na timu za Misri, Algeria, Morocco na Afrika Kusini na kupata changamoto kubwa. Kwa jinsi ninavyoifahamu michuano ya Kombe la Shirikisho huko mbele inavyokuwa, bado Namungo wana kazi kubwa sana ya kuboresha kikosi chao ili kiwaze kupambana.

Mfano tu, kikosi hiki kikikutana na timu kama APR ya Rwanda au Gor Mahia ya Kenya, itakuwa shughuli pevu, bado Al Rabita haiwezi kuwa kigezo cha Namungo kuridhika kuwa ina timu ya kucheza Kombe la Shirikisho.

Bado kuna kazi kubwa ya kufanya ya kukiboresha kikosi hicho ili kiweze kupambana haswa na miamba ya soka Afrika ambao wengine bado wanasubiri kwenye raundi ya kwanza, na baadhi watadondoka kutoka kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kinachotakiwa kufanywa kwanza ni kutafutwa straika wa kumsaidia Sey ambaye anaonekana kama yeye peke yake ndiye anayepambana mbele tofauti na Bigirimana Blaise ambaye msimu huu anaonekana bado hayupo vizuri, lakini viungo wa Namungo hawajaweza kufanya kazi vizuri ya kuwaunganisha mabeki na washambuliaji.

Sehemu ambayo unaweza kusema Namungo ipo vizuri zaidi ni eneo la golikipa. Jonathan Nahimana ni kipa mwenye viwango vya kucheza michuano ya kimataifa kama Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, hivyo sasa wanatakiwa watafutiwe watu wa kufanya naye kazi ili Namungo itishe kwenye michuano hiyo mwaka huu.

Hii ni michuano ambayo kila timu inaposonga mbele ndipo inakutanga na changamoto kubwa zaidi, hivyo inabidi timu kujipanga kikamilifu.



Baadhi ya wanachama wa kikundi kinachojishughulisha na kilimo cha Nguvukazi kutoka Kijiji cha Rusoli, wilayani Musoma mkoani Mara, wakihudumia shamba lao la mahindi juzi, ambalo wamelima kwa kutumia jembe la kukokota na ng'ombe ambalo ni miongoni mwa yaliyotolewa msaada na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Meneja Finca, wenzake kortini tuhuma za wizi

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

WAFANYAKAZI wanne wa Benki ya Finca Tawi la Geita, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita kwa makosa mawili ya wizi wa Sh. milioni 33.

Wanadaiwa kuwa wakiwa na nia ya kudanganya, waliwasilisha ripoti za uongo za kimahesabu, ambapo ripoti yao ilionyesha kwamba salio lililokuwapo kwenye benki yao katika mahesabu ilikuwa Sh. 76,880,300 wakati uhalali ni Sh. 47,880,300 kinyume cha kifungu cha 317 (b) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura ya 16 marejeo ya mwaka 2019.

Washtakiwa hao waliofikishwa mahakamani ni Maria Mwakapala (32) wa kitengo cha mapokezi benki ya Finca, Philip Dahaye (35), mhasibu, Francis Kazaura (39), Meneja na Furaha Twinzi (21) ambaye ni mlipaji mkuu wa benki hiyo.

Washtakiwa wote kwa pamoja walipandishwa kizimbani Ijumaa mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Obadia Bwegoge na waliwasomea mashtaka yao mawili, lakini waliyakana.

Washtakiwa wako nje kwa dhamana ya wadhamini wawili wawili, ambao walitoa barua za utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 4 kwa kila mdhamini.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Masambu Danieli, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo namba 376/2020 umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali.

Hakimu Bwegoge alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Desemba 10, mwaka huu kwa ajili ya kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Masambu Danieli alidai kwa tarehe tofauti na muda kati ya Januari na Mei mwaka huu, katika Benki ya Finca Tawi la Geita katika Wilaya na Mkoa wa Geita, washtakiwa wakiwa waajiriwa wa Benki ya Finca, waliiba kiasi cha Sh. milioni 33 mali ya benki hiyo.

Danieli aliendelea kudai kuwa kosa la pili washtakiwa wote kwa pamoja wakiwa na nia ya kudanganya, waliwasilisha ripoti za uongo za kimahesabu, ambapo ripoti yao ilionyesha kwamba salio lililokuwamo kwenye benki yao katika mahesabu ilikuwa ni Sh. 76,880,300 wakati uhalali ni Sh. 47,880,300 kinyume cha sheria.

# Serikali yasisitiza miradi kutatua migogoro ya wakulima, wafugaji

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema katika kuboresha na kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo Mkoa wa Morogoro, imeendelea kusisitiza uwapo wa miradi ambayo itakuwa na manufaa makubwa kwa makundi hayo mawili.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, aliyasema hayo alipotembelea ujenzi wa mradi wa kiwanda cha nyama katika Ranchi ya Nguru Hills mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki.

Alisema mradi huo unaotarajia kukamilika Aprili mwaka 2021, utakuwa na manufaa makubwa kwa wafugaji na wakazi wa mkoa wa Morogoro.

Prof. Gabriel alisema kuwa mradi huo wa kipekee, baada ya kiwanda hicho kukamilika, kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe zaidi ya 200 na mbuzi 1,000 kwa siku.

Alisema tayari kumejengwa mabwawa makubwa ambayo yatakuwa yanakusanya maji yanayotoka kwenye machinjio na kuyatibu kabla ya kutumika tena kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

Prof. Gabriel alisema mradi huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 25, ambao unashirikisha wabia mbalimbali ukiwamo Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), ni azma ya serikali katika kuboresha mazingira ya uwekezaji hapa nchini.

Alisema kupitia mradi huo, wafugaji wataboresha mifugo yao kwa kufuga ng'ombe bora wa kisasa na kuinenepesha ili iwe yenye ubora.

Pia alisema utasaidia katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo hapa nchini kwa lengo la kukuza pato la nchi kupitia uchumi wa viwanda.

Prof. Gabriel alilitaka dawati la sekta binafsi lililo chini ya wizara hiyo, pamoja na idara ya uzalishaji na masoko kwa kushirikiana na PSSSF kukutana haraka ili kujadili changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika mradi wa kiwanda cha nyama Nguru Hills ili mradi huo ukamilike kwa wakati.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Hassan Chama, alimhakikishia Katibu Mkuu huyo kuwa kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wafugaji na kuwaondolea changamoto ya kuuza mifugo yao kupitia minada ambayo wamekuwa wakikutana na madalali ambao wanafanya bei za mifugo kuwa chini.

Mradi wa kiwanda cha nyama katika Ranchi ya Nguru Hills unaotarajia kukamilika Aprili mwakani, unategemewa kutoa ajira kwa wafanyakazi 120 hadi 200 kulingana na uzalishaji.

# NMB kinara wa kusaidia huduma za kijamii Ilala

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya NMB imepewa cheti kuwa taasisi kinara ya kifedha katika Manispaa ya Ilala katika mkoa wa Dar es Salaam inayotumia kiasi kikubwa cha pato lake kuisaidia jamii katika sekta za elimu, na afya kupitia mpango wake wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR).

Pia, imekuwa kinara kati ya taasisi nyingi za fedha ambayo imekuwa ikishirikiana na serikali kuhakikisha huduma bora za kiafya na elimu zinapatikana kwa wananchi katika mkoa huo.

NMB ilipata cheti hicho kwenye hafla ya kufunga kongamano la siku ya mlipakodi lililofanyika mwishoni mwa wiki.

Katika hafla hiyo manispaa hiyo ilikabidhi vyeti kwa taasisi, mashirika, kampuni na wafanyabiashara 100 bora wa ulipaji kodi bila shuruti, huku NMB ikipongezwa na kutunukiwa kama kinara wa matumizi ya pato lake katika kusaidia jamii.

Akizungumza katika kongamano hilo, ofisa miradi wa masuala ya uwajibikaji kwa jamii wa benki hiyo, Lilian Kisamba, alisema mwaka huu benki hiyo imetoa Sh. milioni 218.9 katika mkoa wa Dar es Salaam, upande wa miradi inayogusa jamii moja kwa moja.

Alisema kuwa kati ya fedha hizo, Sh. milioni 153.9 zimetumika katika sekta ya elimu na Sh. milioni 65 ikienda kwenye afya, na kwamba jumla ya shule 26 zimepokea madawati 300 na kusaidia watoto 3,900 ambao walikuwa wanakaa chini kwa kukosa madawati.

Pia, alisema benki hiyo imetoa misaada mingine ya bati zenye thamani ya Sh. milioni 40 kwa shule sita katika mkoa huo wa Dar es Salaam.

Meneja Mwandamizi wa Idara ya Huduma za Serikali wa NMB, Adelard Mang'ombo, alitumia hafla hiyo, kuwahakikishia wafanyabiashara kuhusu uwapo wa mikopo ya haraka yenye riba nafuu, pamoja na elimu inayohusu masuala ya kifedha kwa ustawi wa biashara zao.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilubuzu Ludigija, alilipongeza Baraza la Wafanyabiashara Tanzania kutokana na mwelekeo chanya wa ulipaji kodi miongoni mwa wafanyabiashara, huku akiwaahidi msaada katika mahitaji ya uanzishaji na uendelezaji wa biashara zao.

Ludigija alisema serikali inajivunia wafanyabiashara wanaolipa kodi bila shuruti katika manispaa yake, huku akiitaja NMB kuwa imefanya msaada mkubwa kwa serikali katika makusanyo ya kodi na mapato.

# JPM aanza uteuzi nafasi zake 10

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli (pichani), ameanza uteuzi wa nafasi zake 10 za wabunge kwa mujibu wa Katiba, kwa kumteua Katibu wa Halmashuri Kuu (NEC), Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, kuwa mbunge.

Sehemu ya pili ya Katiba inayozungumzia wabunge, Ibara ya 66 (1) (e), inatoa mamlaka kwa rais kuteua wabunge wasiozidi 10 kutoka miongoni mwa watu wenye sifa.

"Wabunge wasiozidi kumi waliteuliwa na rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa kwa mujibu wa ibara ya 67 isipokuwa sifa iliyotajwa katika ibara ya 67 (1) (b),"

Ibara ya 67 (1) inasema "Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara hii, mtu yeyote atakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteulia kuwa mbunge endapo; (a) ni raia wa Jamhuri ya Muungano aliyetimiza umri wa miaka 21, na ambaye anajua kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza.'"

Katika uteuzi huo, rais pia amemteua Riziki Saud Lulida, ambaye katika bunge lililopita alikuwa Mbunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), ambaye Juni mwaka huu, aliomba kurudi CCM.

"Wabunge wateule hao wataapishwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," ilisema sehemu ya taarifa hiyo iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Ikulu, Gerson Msigwa.





Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (kulia), akiwa na Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Jenista Mhagama, wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa tangi la maji kijiji cha Nakahuga, Halmashauri ya Wilaya ya Songea.
**PICHA: MPIGAPICA WETU**

# Arusha yapata meya mpya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha limepata meya mpya, Maxmilian Irange, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Naibu Meya wa Jiji hilo, Veronica Hosea.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi wa meya huyo, Katibu Tawala Wilaya ya Arusha, Nyangusi Naibala, alisema Irange ambaye ni meya alipata kura 32 huku kura moja ikiwa imeharibika na kufanikiwa kupata nafasi hiyo.

Naibu Meya alipata kura 32 kati ya kura 33 zilizopigwa huku kura moja ikiharibika.

Wakitoa neno la shukrani, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Arusha, Joseph Massawe, alisema walilima mashamba wakapalilia na kuvuna hivyo siku ya mavuno ni kushangilia.

Aliwapongeza madiwani hao kwa kuchaguliwa na hawakukosea hata mmoja kuchaguliwa kwa sababu walipimwa na kufanyiwa tathmini na kuonekana wanatosha katika kata na viti maalum.

"Nawapongeza Naibu Meya Veronica kwa kuchaguliwa kupata nafasi hiyo na meya pia na naomba madiwani mtambue uchaguzi umeisha na kama hujachaguliwa katika kamati mbalimbali au madaraka fulani msilazimishe jambo," alisema na kuongeza:

"Tunaamini kwa Arusha ya sasa vurugu basi sababu tunadiwani mmoja kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), huku nyie mpo 24 hivyo nawaomba mpeni ushirikiano huyu mtoto wa dawa aliyetoka upinzani," alisema.

# UTT yazindua huduma mpya

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Uwekezaji ya UTT AMIS imezindua rasmi huduma ya usimamizi wa fedha (UTT AMIS – Wealth Management Services) kwa ajili ya wawekezaji wenye kipato kikubwa.

Huduma hiyo ina lengo la kuwezesha wawekezaji hao au taasisi kuwekeza maeneo mahususi kulingana na matakwa yao.

Mkurugenzi Mkuu wa UTT AMIS, Simon Migangala, alisema huduma hiyo imeanzishwa ili kukidhi mahitaji maalum ya wawekezaji ambao kwa namna moja au nyingine hayapatikani katika mifuko mingine ya uwekezaji wa pamoja inayoendeshwa na kampuni hiyo.

Migangala alisema hayo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa mikutano ya mwaka wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja inayoendeshwa na UTT AMIS, na kusema huduma hiyo imekuwa ikitolewa kwa wawekezaji mbalimbali kabla ya uzinduzi na mpaka sasa ina kiasi cha Shilingi bilioni 16.

"Moja ya malengo ya UTT AMIS ni kuendeleza na kubuni bidhaa na kutoa huduma zinazokidhi mahitaji mbalimbali ya wawekezaji katika masoko ya fedha na mitaji hapa nchini ili kuendelea kuwa mshirika hakika katika uwekezaji," alisema Migangala.

Aliongeza kuwa UTT AMIS ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, na kwa sasa ina simamia mifuko sita ya uwekezaji ambayo ni Umoja, Wekeza Maisha, Watoto, Kujikimu, Ukwasi na Mfuko wa Hatifungani (Bond Fund).

Alisema kuwa mifuko hiyo inaendelea kuwawezesha Watanzania kuweka akiba na kunufaika na uwekezaji katika masoko ya fedha na mitaji, hivyo kuendelea kutimiza azma ya serikali ya kuendelea kuwawezesha wananchi kunufaika na fursa za uwekezaji.

Migangala, alizitaja faida za kuwekeza kwa kutumia huduma hiyo (UTT AMIS – Wealth Management Services) kuwa ni kupata mapato na ukwasi kwa kuzingatia aina ya uwekezaji, utaalamu wa uwekezaji utakaotatua na kuhusisha mahitaji ya pesa na uwekezaji kwa ufanisi, mseto wa uwekezaji kwenye masoko ya fedha na mitaji na kupata taarifa ya uwekezaji kulingana.

# Zaidi ya mil. 200/- zakusanywa kwenye misitu

**Na Lulu George,** RUANGWA

ZAIDI ya Sh. milioni 279 zimekusanywa katika Kijiji cha Nandenje, Kata ya Mandarawe, Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi ikiwa ni mapato ya mazao ya misitu.

Fedha hizo zimekusanywa katika kipindi cha miaka mitano toka 2015 hadi 2020 na zimefanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ya kijiji hicho ikiwamo ujenzi wa zahanati, nyumba ya mganga, shule ya sekondari na nyumba mbili za walimu.

Shughuli nyingine ni pamoja na ununuzi wa trekta, ujenzi wa jengo ka kuhifadhia trekta pamoja na ujenzi wa choo cha zahanati.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Nandenje, Rashid Kajete, alisema hayo wakati alipokuwa akizungumza na waandishi walio kwenye ziara ya mafunzo ya uandishi wa habari za uchunguzi kuhusu mazao ya misitu kutoka mikoa ya Tanga, Lindi, Ruvuma na Morogoro yaliyoratibiwa na Mradi wa Mnyororo wa Thamani wa mazao ya misitu (FORVAC).

Kajete alisema kijiji hicho ni miongoni mwa vijiji vitano vilivyopo chini ya FORVAC ambavyo vimeonyesha mafanikio makubwa ya kiuchumi kutokana na uvunaji wa mazao ya misitu.

Alisema mafanikio hayo yametokana na utekelezaji wa sera ya misitu ya mwaka 1998 inayotoa kipaumbele kwa jamii kushirikishwa katika usimamizi wa misitu kwa lengo kukuza kipato cha jamii ili kupunguza umaskini.

Alisema katika kipindi hicho, Halmashauri ya Ruangwa ilikusanya zaidi ya Sh. milioni 47.9 na kamati ya misitu ya kijiji hicho ilikusanya Sh. milioni 153.

Mtendaji huyo alisema, kijiji hicho kina watu 2,200 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 na kina ukubwa wa hekta 12,745.48, kati ya hizo 5,025 ni hifadhi ya misitu.

"Pamoja na kijiji kutenga msitu wa hifadhi, lakini kuna mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji na makazi ya watu na mpango wa uhifadhi wa misitu ulianza mwaka 2004 na kufanyiwa mapitio mwaka 2014 na kwa kweli tumeona mafanikio makubwa sana," alisema.

Alitaja aina ya miti inayovunwa na kuuzwa kuwa ni pamoja na msekeseke, mninga, mtondolo, mnangu na mkongo.

Baadhi ya wananchi walieleza mafanikio hayo kuwa ni ukombozi mkubwa ndani ya kijiji hicho.

Ofisa misitu wa Wilaya ya Ruangwa, James Kabuta, alisema halmashauri hiyo inachukua asilimia 10 ya mapato yote ya mazao ya misitu kutoka kwenye kijiji na asilimia 60 inakwenda kijijini, 30 inapelekwa kamati ya misitu ya kijiji.

Msimamizi wa wataalamu wa misitu wa mradi wa FORVAC, Alex Njahani, alisema mradi huo unatekelezwa katika halmashauri 10 za wilaya nchini kutoka mikoa ya Dodoma, Tanga, Lindi, Ruvuma, Dar es Salaam na Manyara.

Njahani alisema halmashauri hizo ni zenye misitu aina ya miyombo na umelenga kuwanufaisha wananchi kwa kutumia maliasili zilizopo kwenye maeneo yao ili kuongeza kipato.

Alisema kwa sasa FORVAC unalenga kutoa elimu ya biashara, ili kumnufaisha mwananchi mmoja mmoja kwa kutumia uhifadhi endelevu wa mazao ya misitu.

Misitu ya Miyombo ni aina ya miti inayoota tena baada ya kukatwa na ipo kwenye maeneo mengi nchini.

# Miradi mikubwa ya serikali yanenepesha viwanda saruji

**Beatrice Moses**

MIRADI mikubwa ya ujenzi wa maeneo mbalimbali ikiwamo miundombinu inayotekelezwa chini ya usimamizi wa serikali ya awamu ya tano inatajwa kuwa ni neema ya pekee kwa baadhi ya viwanda vya saruji nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam kuhusu hali ya biashara ya kianda cha saruji Tanga, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Tanga Cement, Lawrence Masha, alisema chini ya uongozi wa Rais John Magufuli wameona manufaa ya miradi hiyo kwa namna tofauti kwani pamoja na kuwanufaisha wananchi , pia imewawezesha kupokea mahitaji mengi ya saruji.

"Juhudi za serikali kukuza uchumi kupitia maendeleo ya miundombinu na ukuzaji wa viwanda vya ndani, vitakuza uzalishaji na matumizi ya saruji ya ndani, wakati ikipunguza ongezeko la uingizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi," alisema Masha.

Alitaja kuwa kufufuliwa kwa reli ya kaskazini imewawezesha pia kusafirisha saruji yao vizuri na kufikisha kwenye masoko husika, hivyo kampuni ina matumaini chanya yanayotokana na mipango ya maendeleo ya miundombinu chini ya Programu ya Maendeleo ya Serikali ya mwaka 2025.

"Tunatarajia miradi mingi kuendelea kushika kasi ndani ya mwaka 2020, kampuni ina uwezo wa kukidhi mahitaji ya saruji nchini kwa kiwango kikubwa, ina ahidi kuzalisha bidhaa za saruji zenye ubora," alisema Masha ambaye ni wakili.

Alizungumzia pia mabadiliko ya soko ya saruji katika hali ya kiushindani katika kipindi cha mwaka cha mapitio yaliyoathiri matokeo ya utendaji wa kifedha kwenye kampuni, yaliongezeka kutokana na mauzo yaliongezeka kwa asilimia 3 na kufikia shilingi bilioni 221 kutoka shilingi bilioni 215 wa mwaka 2018 .

Masha alibainisha kuwa kampuni iliirekodi hasara baada ya shilingi bilioni 12 kwa 2019 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11 za mwaka 2018.

Alisema fedha taslimu iliyopatikana kutokana na shughuli za kibiashara iliongezeka kwa asilimia 4 kutoka shilingi bilioni zilizorekediwa mwaka 2018 na kufikia shilingi bilioni 43 mwaka 2019.

Alibainisha kuwa mtiririko wa fedha kutokana na uendeshaji iliongezeka kwa asilimia 1 kutoka shilingi bilioni 40 ya mwaka 2018 na kuwa shilingi bilioni 41 mwaka 2019, hali mbayo inadhihirisha kuwa misingi ya uendeshaji na mtazamo kibiashara wa kampuni inafanya kazi vizuri.



Wajumbe wa Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, wakijadiliana mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya elimu na afya wilayani humo. Kamati hiyo iliongozwa na Mwenyekiti ambaye ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Edward Mpogolo. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# Mtandao waombwa kuwasaidia wakulima

**Na Yasmine Protace,**
MKURANGA

MTANDAO wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), Mkoa wa Pwani, umetakiwa kuwasaidia wakulima wa wilaya za mkoa huo, ili kuzalisha zaidi.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbeto Sanga, wakati alipofungua mkutano ulioandaliwa na kuwashirikisha wanachama wake.

Sanga aliutaka mtandao huo, uonyeshe kwa vitendo utetezi wa wakulima wake na vipimo halisi kwenye mazao yao, sambamba na bei nzuri ambayo itachangia kuwaboreshea maisha.

"Nakuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mkuranga uwasimamie maofisa ugani na maendeleo ya jamii, ngazi ya kata waache kushinda ofisini, badala yake waende kwenye vitongoji kutoa elimu ya ugani kwa kuhamasisha wakulima wajiunge kwenye vikundi, ili wafaidike na mikopo inavyotolewa na halmashauri pamoja na taasisi nyingine za kifedha," alisema.

Mwenyekiti wa MVIWATA Taifa, Abdul Gea, alimhakikishia Sanga kuwa wamejipanga, kusambaza mtandao huo katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani, ikiwamo na kujikita mashambani kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji kwa kuwatumia wanasheria wao, ambao hushiriki katika mabaraza ya ardhi.

Mwenyekiti wa Mtandao huo, ambaye anaratibu Mkoa wa Pwani, Mohamed Msumi, alimpongeza Rais John Magufuli, kwa kuwajali wakulima kwa kuwasimamia masoko yao wauze bei nzuri.

# Shule zatakiwa kukata bima kukabili majanga

**Na Enock Charles**

WAMILIKI wa Shule wameshauriwa kukata bima ili kupata nafuu ya haraka pale yanapotokea majanga.

Miongoni mwa majanga ni kuungua moto kwa shule hizo au mabweni ya wanafunzi ili kuepuka kuwachelewesha wanafunzi kuendelea na masomo yao wakati wakikabiliana na athari za majanga hayo.

Ushauri huo umetolewa wakati ambapo imeshuhudiwa matukio mengi ya shule mbalimbali nchini kukumbwa na majanga ya moto yaliyopelekea kuungua kwa majengo ya shule hizo, ikiwamo mabweni ya wanafunzi na kupelekea upotevu mkubwa wa mali za shule pamoja na za wanafunzi.

Akizungumza na waandishi wa habari Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa bidhaa za bima zinazohusisha bima ya nyumba na bima magari, Mkurugenzi wa Kampuni ya Bima ya Sanlam, Khamis Suleiman, aliwataka wamiliki hao kutokuogopa gharama za kukata bima ambazo alidai ni kidogo ikilinganishwa na hasara inayotokea baada ya majanga kama vile moto kutokea katika shule hizo ambao husababisha hasara kubwa.

"Baadhi ya wamiliki wa shule wanaona kuwa kulipa bima ni kama gharama za ziada, hivyo hawaji kukata bima, lakini kwa waliokata bima hawapati shida kulipwa madai yao yanapowatokea majanga ya moto, hivyo kuwa nafuu kwao na wanafunzi wao," alisema Suleiman.

"Sisi hatutafuti sababu za kukwepa madai ya wateja isipokuwa tunatafuta sababu za kulipa madai ya wateja wetu Standard Chartered wameliona hilo na ndio maana tumekuwa wa kwanza katika ya kampuni za bima 31 ambazo zipo sokoni kuingia ubia na benki Standard Chartered," alitamba Suleiman.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani, alisema kuwa mpaka sasa kiwango cha wananchi wanaotumia bidhaa za bima ni wachache ikilinganishwa na wasiokata bima jambo ambalo sio zuri kwa mustakabali wa wananchi.

"Kupitia kwenu tunataka kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa bima, yapo madhara mengi yanayotokea katika jamii kutokana na ukosefu wa bima ambayo yangeweza kuepukwa kama tu wahusika wangekuwa wamekata bima," alisema Rughani.

# Madiwani wapewa jukumu la migogoro wakulima, wafugaji

**Na Shaban Njia,** NGARA

SERIKALI wilayani Ngara Mkoa wa Kagera, imewataka madiwani wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kuhakikisha wanatatua migogoro tija kati ya wafugaji na wakulima katika maeneo yao.

Migogoro hiyo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara na kusababisha kuwapo kwa uvunjifu wa amani.

Luteni Kanali Maiko Mtenjeli, Mkuu wa Wilaya ya Ngara, alitoa kauli hiyo katika kikao maalumu cha kuwaapisha madiwani wapya wa halmashauri hiyo, na kueleza kuwa wafugaji kwa sasa wanalisha mifugo yao katika eneo la Jeshi la Magereza na Hifadhi ya Taifa ya Burigi bila ya kuwa na vibali.

Alisema kuna wafugaji wanalisha mifugo yao katika maeneo yasiyoruhusiwa na kusababisha migogoro, na kuwataka madiwani hao kwenda kushughulikia kero hiyo haraka ili shughuli za uzalishaji mali ziendelee.

"Mnapaswa kwenda kuwaelimisha ili kuachana na tabia hii, ni kinyume cha sheria za nchi...mliomba kazi ya kuwatumikia wananchi, nendeni mkafanye kazi," alisema Mtenjeli. Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Wilbard John Mabara ambaye ni Diwani wa Kata ya Rusumo, alisema katika kutekeleza suala hilo hainabudi wakawashirikisha viongozi wa serikali za vijiji katika maeneo yao ili kupata suluhu ya migogoro hiyo ambao kwa sasa imeanza kufukuta.

Naye Mbunge wa Ngara, Ndaisa George Ruhoro, alisema atahakikisha anatenga siku mbili za kusikiliza kero za wananchi hasa wakulima na wafugaji, na kumwomba mkurugenzi wa halmashauri hiyo,

Aidan Bahama, kumpa ushirikiano katika utatuzi wa migogoro ya wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, akizungumza na Meneja Mwandamizi Idara ya Biashara za Serikali, Adelard Mang'ombo, baada ya kukabidhiwa cheti cha shukrani kwa Benki ya NMB kuwa mmoja wa wadau walipa kodi wakati wa Siku ya Mlipa Kodi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Dar wafunguka katazo vifungashio vya plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

TAKRIBANI wiki moja tangu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kutangaza kwamba utengenezaji, usambazaji na uuzaji wa vifungashio vya plastiki vitakoma ifikapo Desemba 31, mwaka huu, baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam wamekubaliana na hatua hiyo.

Wamesema ni vizuri kuzuia vifungashio hivyo iwapo vinadhuru afya za watu na mazingira.

Wengine wamesema wafanyabiashara waelezwe vifungashio mbadala watavipataje, huku wengine wakisema watengenezaji wa vifungashio halali wafanye bidii kuvifikisha sokoni.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi wengi wahojiwa wamepongeza hatua hiyo, lakini wengine wamehimiza NEMC na taasisi nyingine kuwaeleza wafanyabiashara wadogo mahali pa kupata vifungashio mbadala.

"Katazo lenu hilo sina namna ya kulizuia. Halina maana kama hamsemi tutapata wapi vifungashio halali sisi watu wadogo," ameeleza muuza maji ya kunywa yanayovuma kama 'kandoro', alisema Rehema Mhintiri na kushauri watengenezaji wa vifungashio halali wavifikishe sokoni.

Shukuru Ismail, mkazi wa Tandika, alisema watu wengi hawawezi kutofautisha vifungashio vya plastiki na mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku na serikali.

Alisema kuwa vifungashio hivyo vinachafua mazingira sawa na mifuko iliyokatazwa na kwamba anaona watengenezaji wa vifungashio hivyo wametumia mwanya uliopo kurudisha mifuko ya plastiki kupitia mlango wa nyuma.

"Siku zote nimekuwa nikijiuliza hawa NEMC wapo wapi? Lakini kwa hatua waliyochukua ni madhubuti na itasaidia kuthibiti hata viwanda vya uchochoroni," alisema Ismail.

Erick Shemdolo, muuza maji, alisema hajui vifungashio hivyo vinatengenezwa wapi au nani. "Mifuko hii wanaileta wafanyabiashara wenzetu. Wenyewe wanajua wanaipata wapi. Lakini tunaihitaji kuifanya biashara," alieleza.

Ezekiel Kapinga mkazi wa Boko Kanisani, alilihimiza baraza kusimama kidete kulina sheria iliwapo lina ushahidi wa kitaalamu kwamba vifungashio vya plastiki vinadhuru afya ya mwanadamu. "Sina hakika kama ni vyepesi kuoza, kama ni vitu vya hatari ni muhimu kuzuia matumizi yake; kwa hiyo katazo hili ni zuri na muhimu."

Hashim Mbeleko, muuza ndizi, alisema vifungashio hivyo wanavipenda wateja wake, lakini hajui madhara yake au anavitengeneza nani. "Ndugu yangu mambo hayo siyajui. Nina elimu yangu kidogo inayonisaidia kupata riziki," alieleza.

Hilda Kajaula, mkazi wa Kibada, alieleza kuwa hana ugomvi na katazo hilo isipokuwa dukuduku lake ni kwamba wafanyabiashara hawajaelezwa vifungashio mbadala.

# Red Cross yaahidi makubwa miaka 5

**Na Yasmine Protace**

RAIS wa Tanzania Red Cross Society, David Kihenzi, amesema taasisi yao imejipanga kuendelea kufanya mabadiliko makubwa ya kiutendaji katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Alisema hayo jijini Dar es Salaam katika mkutano uliowashirikisha wajumbe, wenyeviti wa mikoa mbalimbali na Visiwani, wawakilishi wa vijana, watendaji kazi na watendaji wa RedCross Tanzania.

Kihenzi ambaye ni Mbunge wa Mufindi, alisema mikakati hiyo ya miaka mitano ni pamoja na kuwa na programu ya kuwasaidia watoto yatima na wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (HIV).

"Tutawasaidia watoto wawe na maisha bora, tutawasaidia wajiendeleze pale watakaposhindwa kwenda shule, tutawawezesha wajiajiri baada ya kupatiwa mafunzo ya ufundi selemala," alisema.

Aliongeza kuwa mkakati mwingine ni kujikita katika maendeleo ya kiofisi ili taasisi iwe na matawi imara ikiwamo kuwa na watu wa kujitolea walio na weledi. Mkakati mwingine ni kuhakikisha matawi yanakuwa chachu katika changamoto za kijamii.

Pia kuwa na viongozi wanaoelewa majukumu yao, ikiwamo kusimamia shughuli za kitaasisi katika maeneo yao pamoja na maendeleo ya kitaasisi ambapo ni kuhamasisha wananchi ili wapate wanachama ikiwamo kuongeza nguvu ya vijana.

"Vijana wana malengo makubwa kutokana na kuwa na ubunifu," alisema na kuongeza kuwa mkakati mwingine ni matawi kuwa na ofisi na vikosi kazi katika kufanya kazi katika maafa.

Kadhalika wanakusudia kuongeza programu mbalimbali ambapo pia wamejipanga katika kuendelea masuala ya afya.

Kuhusu idadi ya wanachama, alisema katika kipindi cha mwaka jana kulikuwa na wanachama 20,000, lakini kuanzia Januari hadi sasa wamefikia 58,000.

Alisema mpaka sasa kuna vijana wa kujitolea 100,000, na ndio wanaofanya kazi kubwa.

Nipashe
Spotika



NYOTA WA5 WANAOWEZA KUHAMIA EPL JANUARI 2021 UK. 12-13

# WACHEZAJI WA5 EPL BORA ZAIDI KWA KLABU ZAO SASA

**LONDON,** England

LIGI Kuu England bila shaka ndiyo tajiri zaidi katika soka la ushindani duniani. Sio jambo la ajabu kwa wachezaji wengi kutaka kwenda kucheza kwenye ligi hiyo, huku wakipata mishahara mikubwa ambayo nje ya ligi hiyo pengine wasingeweza kupata kiasi hicho cha fedha.

Bila shaka yoyote Ligi Kuu England inajumuisha wachezaji wengi wazuri, lakini kiwango cha mchezaji mwenyewe ndicho kinachotoa nafasi kwake kwenda kucheza kwenye ligi hiyo. Makala haya yanawachambua wachezaji watano bora zaidi katika klabu zao kwa sasa, ambao wapo kwenye kiwango bora, lakini hawapo kwenye mpangilio maalumu...

**#5. Jack Grealish (Aston Villa)**

Jack Grealish amekuwa mchezaji mwenye kiwango cha kuvutia zaidi pale Aston Villa. Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 25, amecheza zaidi ya mechi 30 za Ligi Kuu kwa Aston Villa msimu uliopita, akifunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho sita, baada ya kuisaidia klabu hiyo kupanda kwenye Ligi Kuu msimu wa 2018-19.

Msimu huu, Grealish amekuwa kwenye kiwango bora zaidi. Tayari amefunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho sita katika mechi nane za Ligi Kuu. Grealish aling'ara wakati Villa ikiitenda vibaya Liverpool kwa kuichapa mabao 7-2.

Shukrani kwa kiwango chake, Grealish ameichezea kwa mara ya kwanza timu ya Taifa ya England msimu huu. Ingawa bado hajaifungia bao, lakini tayari ana pasi za mwisho mbili. Kama ataendelea kuwa kwenye kiwango hiki bora kwa klabu na nchi yake, halitakuwa jambo la kushangaza kuona Grealish akinyakuliwa na klabu kubwa.

**#4. Wilfried Zaha (Crystal Palace)**

Wilfried Zaha amekuwa mchezaji muhimu kwa Crystal Palace kwenye Ligi Kuu kwa miaka sasa. Straika huyo mwenye umri wa miaka 28 raia wa Ivory Coast, angalau amechangia mabao kumi katika mechi tatu zilizopita kati ya nne za Ligi Kuu, kiwango ambacho kimevutiwa na klabu kubwa.

Zaha alikuwa akihusishwa sana na kuondoka pale Palace kipindi cha majira ya joto, lakini hilo halikutokea kwa sababu hakuna klabu iliyofikia bei waliyokuwa wakiitaka Crystal Palace kwa mchezaji huyo.

Msimu huu, Zaha tayari amefunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi nane za Ligi Kuu kwa Crystal Palace, ambayo imekaa karibu na Manchester United, Arsenal na Manchester City kwenye msimamo wa ligi.

Huku akiwa anatajwa kuwaniwa na klabu kubwa katika dirisha dogo la usajili la Januari, Zaha anaweza asikae kwa muda mrefu pale Palace licha ya klabu hiyo kutaka kiasi kikubwa cha fedha.

**#3. Pierre-Emerick Aubameyang (Arsenal)**

Pierre-Emerick Aubameyang amekuwa mmoja wa wachezaji ambaye amekuwa kwenye kiwango kizuri tangu alipotua Arsenal mwaka 2018. Mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, hakuchukuwa muda mrefu kuonyesha kiwango chake kwa klabu yake hiyo mpya, akifunga mabao kumi katika nusu ya msimu wa 2017-18 kwenye Ligi Kuu England.

Straika huyo wa kimataifa wa Gabon, akafunga mabao 22 kwenye msimu uliofuata na kushinda Kiatu cha Dhahabu. Hata hivyo, licha ya kiwango cha Aubameyang, Arsenal ilishindwa kumaliza kwenye nne bora katika misimu yote miwili.

Mfungaji huyo bora wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu wa 2016-17 ni mchezaji mzuri, lakini ameshindwa kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Baada ya mechi tisa, Arsenal wapo nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu (Kabla ya mechi za mwishoni mwa wiki). Licha ya mchezaji huyo hivi karibuni kukubali kuongeza mkataba mpya wa kubaki katika klabu hiyo, anaonekana hataweza kubaki hapo Arsenal baada ya msimu huu kama miamba hao wa London hawatafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#2. Danny Ings (Southampton)**

Jambo lililowazi kwamba, Danny Ings amekuwa mchezaji muhimu kwa Southampton kwenye Ligi Kuu.

Mshambuliaji huyo wa kati mwenye umri wa miaka 28, amefunga karibia asilimia 50 (mabao 22) ya Southampton kati ya 51 ya Ligi Kuu msimu wa 2018-19.

Ings pia ameendelea kuwa na kiwango cha kuvutia msimu huu, akifunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi saba za Southampton ambao wapo nafasi ya saba baada ya mechi saba.

Vinara wa ligi hiyo Tottenham Hotspur (kabla ya mechi ya jana) wameripotiwa kuhitaji huduma yake, unaweza kuwa muda mzuri kwa Ings kwenda kucheza katika klabu kubwa.

**#1. James Rodriguez (Everton)**

Real Madrid imeonekana kumkataa James Rodriguez ambaye sasa yupo kwenye maisha mapya baada ya kuungana na kocha wake wa zamani, Carlo Ancelotti pale Everton kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Mshindi huyo wa Kiatu cha Dhahabu kwenye Kombe la Dunia mwaka 2014 nchini Brazil, ameng'ara kwenye Ligi Kuu ya England, akifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho nane, baada ya kushindwa kutamba kwa miamba wa Ligi Kuu ya Hispania.

Inaeleweka kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye bado yupo kwenye kiwango chake, anaonekana kuendelea kuwa chaguo la kwanza hapo Everton baada kukalia benchi kwa muda mrefu kule Real Madrid.

Kama ataendelea kuwa katika kiwango hiki bora pale Everton, halitakuwa jambo la ajabu kuona James akinyakuliwa na klabu kubwa.

## ISIKUPITE

TANGU alipocheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu England (akiwa Chelsea Agosti 2013), Kiungo wa Manchester City, Kevin De Bruyne, ametoa pasi za mwisho [assists] 71 kwenye ligi hiyo, ambazo ni nane zaidi ya zilizotolewa na mchezaji yeyote katika ligi hiyo, licha ya kucheza mara tatu tu katika misimu yake miwili ya mwanzo kwa wakati huo.



Extra Time

# NYOTA WA5 WANAOWEZA KUHAMIA EPL JANUARI 2021



KOULIBALY

**LONDON,** England

MSIMU wa 2020-21 kwenye Ligi Kuu England, EPL, umekuwa wa kuvutia kwa njia nyingi. Katika mwaka ambao kumekuwa na mlipuko wa virusi vya corona, Ligi Kuu England kama ligi nyingine nyingi za soka duniani, ilichelewa kumalizika msimu uliopita.

**Hiyo maana yake ni kwamba msimu mpya wa Ligi Kuu umekuja muda mfupi tu baada ya ule mwingine kumalizika.**

Miamba wawili wa hivi karibuni kwenye Ligi Kuu ya England, Manchester City na Liverpool - imeonekana kuwa kwenye wakati mgumu na tayari zimechezea vichapo.

Hata timu nyingine kubwa kwenye ligi hiyo kama vile, Manchester United, Chelsea, Arsenal - zimekuwa na mwanzo wa tofauti kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Manchester United haijashinda katika mechi zake nne za mwanzo za ligi msimu huu ikiwa ni kwa mara ya kwanza kwa zaidi ya miongo mitano iliyopita.

Kikosi cha gharama kubwa, Chelsea ndicho kimeanza kurudi kwenye mstari wake, huku Arsenal ya Mikel Arteta tayari imechezezea vichapo mara nne kwenye ligi msimu huu.

Baada ya ratiba ngumu kwa ligi za nyumbani, klabu za Ligi Kuu England pia zipo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi ya Europa.

Hata hivyo, baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa, timu nyingi za Ligi Kuu zimekuwa na majeruhi ya wachezaji wake muhimu. Kutokana na hilo, usajili wa dirisha la Januari unaweza kuwa muhimu mno kwa timu hizo kuimarisha vikosi vyao.

Katika makala haya, tunaangalia wachezaji watano ambao wanaweza kuhamia kwenye Ligi Kuu ya England wakati wa dirisha la usajili mdogo wa Januari, hawa hapa...

## #5. ISCO

Tangu kuwasili Real Madrid kipindi cha majira ya joto mwaka 2013, kiungo huyo wa zamani wa Malaga, Isco ameshinda mataji 16 yakiwamo mawili ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, tangu kurudi kwa Zinedine Zidane katika kipindi chake cha pili kama kocha wa Real Madrid, Isco mwenye umri wa miaka 28, amekuwa hana nafasi tena pale Santiago Bernabeu. Tangu mwanzo wa msimu wa 2019-20, Isco amefunga mabao mawili tu katika mechi 30 za mashindano yote.

Real Madrid inaonekana kuwa tayari kusikiliza ofa kwa Isco, ambaye amekuwa akitajwa kuwaniwa na klabu mbili za Ligi Kuu ya England - Arsenal na Everton.

Everton pia imeonyesha nia ya kutaka kumsajili Isco ambaye anaweza kwenda kuungana na kocha wake wa zamani hapo Real Madrid, Carlo Ancelotti na mchezaji mwenzake wa zamani, James Rodriguez.

Ukichukulia ubora wake, Isco anaweza kuwa na mchango mkubwa kwa klabu yoyote itakayoweza kupata saini yake kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu.

## #4. DOMINIK SZOBOSZLAI

Kiungo wa Salzburg, Dominik Szoboszlai amevutia hisia kwa timu nyingi za Ulaya kama vile Real Madrid, Bayern Munich, Arsenal na Everton.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 raia wa Hungary, tayari amefunga mabao 22 na kutoa pasi za mwisho 33 tangu awasili hapo kutoka klabu ya nchini Austria akiwa mchezaji huru mwaka 2018. Pia amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia kwa nchi yake - bao la ushindi la dakika za mwisho la Szoboszlai dhidi ya Iceland, liliiwezesha Hungary kufuzu kucheza michuano ya Euro 2020 itakayofanyika mwakani.

Szoboszlai amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia msimu huu wa 2020-21 - amefunga bao na kutoa pasi za mwisho sita. Na sasa mchezaji huyo anatajwa kwamba, anakaribia kuondoka kwenye Ligi Kuu Austria na Arsenal imekuwa ikihusishwa zaidi kuwania saini ya kiungo huyo.

Salzburg wamekuwa na rekodi nzuri ya hivi karibuni kwa kutoa vipaji kama Sadio Mane na Takumi Minamino, ambao wanang'ara sasa kwenye Ligi Kuu ya England. Szoboszlai anaweza kuwa anaelekea mweleko huo huo kwenda katika klabu kubwa.

Mchezaji huyo ambaye tayari amekuwa akifananishwa na gwiji wa Hungary, Ferenc Puskas, anaweza kutua Arsenal Januari.

## #3. KALIDOU KOULIBALY

Kalidou Koulibaly wa Napoli amekuwa mmoja wa walinzi bora zaidi Ulaya tangu kutua kwake kule Kusini mwa Italia wakati wa kipindi cha majira ya joto mwaka 2014.

Mlinzi huyo wa kati mwenye umri wa miaka 28 raia wa Senegal, ambaye thamani yake inatajwa kuwa ni euro milioni 65, amekuwa moyo wa ulinzi wa Napoli, akicheza zaidi ya mechi 250 kwenye mashindano yote pia akifunga mabao 10 na kutoa pasi za mwisho tano.

Koulibaly alikuwa akihusishwa sana kuhamia kwenye Ligi Kuu ya England kipindi kilichopita cha majira ya joto, huku klabu kama Manchester United, Manchester City na Liverpool zote zikionyesha nia ya kutaka huduma yake. Ingawa amebakia pale kwenye mji wa Naples mwanzoni mwa msimu huu, inawezekana kabisa akaenda kwenye Ligi Kuu ya England.

Liverpool imekuwa ikitajwa kumwania baada ya kuumia kwa walinzi wao, Virgil van Dijk na Joe Gomez. Koulibaly anaweza kuwa mrithi sahihi wa mholanzi huyo.

Licha ya kuwaniwa na miamba hao wa Ligi Kuu ya England, Mkurugenzi wa soka wa Napoli, Cristiano Giuntoli hataki kuona Koulibaly akiondoka kwa urahisi.

## #2. DAYOT UPAMECANO

Licha ya umri wake mdogo, Dayot Upamecano amekuwa mmoja wa wachezaji wenye kiwango cha kuvutia zaidi pale RB Leipzig tangu kuwasili klabuni hapo msimu wa 2016-17.

Mlinzi huyo wa kati mwenye umri wa miaka 22, tayari amecheza mechi 120 katika mashindano yote kwa klabu hiyo. Amekuwa na kiwango bora zaidi msimu huu akiibeba Leipzig.

Upamecano alikuwa akihusishwa sana kuhamia Ligi Kuu England kipindi cha majira ya joto, huku Manchester United ikiwania pia saini yake. Lakini mabingwa wa ligi hiyo, Liverpool wametajwa kuwania huduma ya raia huyo wa Ufaransa.

Huku Leipzig ikiwa tayari kusikiliza ofa kwa mlinzi wake huyo ambaye anatajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 40, Upamecano ana uwezekano mkubwa wa kutua kwenye Ligi Kuu ya England Januari, wakati United na Liverpool zikihitaji kuimarisha safu zao za ulinzi.

## #1. OUSMANE DEMBELE

Mmoja wa wachezaji ambao walitambulika kama 'mti uliokufa' pale Barcelona kipindi cha majira ya joto, Ousmane Dembele ambaye alionekana kuelekea Manchester United kabla ya uhamisho huo kushindikana.

Licha ya kutokuwapo kwenye mipango ya Ronald Koeman, mchezaji huyo alibaki Camp Nou na sasa anaonekana kama anaweza kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha kocha huyo. Wakati wakiwa kwenye mdororo wa uchumi, Barcelona wanahitaji kuuza wachezaji ili kupata fedha za kumnunulia Memphis Depay.

Tangu kuwasili katika klabu hiyo ya Catalunya baada ya kutoka kule Borussia Dortmund, raia huyo wa Ufaransa ameshindwa kufikia matarajio yake. Baada ya kuwa nje ya dimba kwa miezi kumi, Dembele alirudi Barcelona Septemba, lakini hajaweza kurejea kwenye kiwango cha kuvutia.

Majeruhi ya mara kwa mara yamekuwa yakimwandama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

Na wakati Man United ikionekana kuwania huduma ya mchezaji huyo, pia Arsenal imeripotiwa kumwania Dembele na anaweza kuondoka pale Barcelona kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari na kutua Ligi Kuu England.

Kama hilo halitatokea kwa Barcelona kumuuza, wanaweza kumpoteza Dembele, kwani atakuwa huru wakati wa kipindi cha majira ya joto.

## Nukuu

"Nimemwona mchezaji atakayerithi nafasi yangu katika soka la Argentina na jina lake ni Messi. Messi ni mwenye uwezo wa hali ya juu," **Diego Maradona enzi za uhai wake.**



"Nilizungumza na Leo [Messi] wakati nilipokuja na aliniambia ilimuumiza wakati nilipokata kuja hapa mara ya kwanza, kwa sababu alitamka hadharani na mimi nikasema hapana, na akaniambia atakufa pamoja na mimi kwa sababu watu wanazungumza vibaya na tumeendelea kuwa na mahusiano mazuri tu," **mshambuliaji wa Barcelona, Antoine Griezmann, akizungumzia uhusiano wake na Messi.**



"Kutoka ndani ya moyo wangu nilikuwa ninapenda kuondoka [Man United] na kujiunga Barcelona. Nilikuwa shabiki mkubwa wa Barcelona kuliko Real Madrid. Nakumbuka niliwahi kukaa chini nikafikiria kwamba ingekuaje ningecheza timu moja na Messi, Xavi, Iniesta na Busquets, na zama zile Messi hakuwa anacheza kama anavyocheza sasa kama namba 9," **nyota wa zamani wa Manchester United, Wayne Rooney.**





Mfungaji wa bao pekee la Yanga dhidi ya JKT Tanzania, Deus Kaseke, akiukwamisha mpira kimyani wakati wakishinda 1-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA INAVYOOKOTA MOJA MOJA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

INAONGOZA Ligi Kuu Tanzania Bara kwa pointi 31, ikiwa imecheza jumla ya mechi 13, imeshinda michezo tisa na sare nne, huku ikiwa haijapoteza hata mechi moja.

**Hiyo ni timu ya Yanga ambayo msimu huu imeonekana kupania kutwaa ubingwa ambao imeukosa kwa misimu mitatu sasa, mbele ya mahasimu wao wa jadi, Simba walioutwaa misimu mitatu mfululizo.**

Wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wanaamini kuwa huu ni msimu wao kutokana na aina ya usajili walioufanya msimu huu.

Hata hivyo, baadhi ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo pamoja na ushindi wote huo, wamekuwa na wasiwasi na aina ya ushindi ambao wamekuwa wakiupata.

Si hao tu, hata Kocha Mkuu wa timu hiyo, Cedric Kaze ameeleza kutoridhishwa na ushindi ambao timu yake imekuwa ikiupata na akaahidi taratibu atakuwa akilifanyia kazi tatizo hilo.

"Kushinda bao moja ni presha tupu, unakaa na wasiwasi hadi mwisho wa mchezo ndiyo unashusha pumzi," amekuwa akieleza Kaze pindi anapoulizwa mara kwa mara timu yake kushinda bao moja.

Baadhi ya mashabiki wa Yanga wanataka kipindi cha dirisha dogo, klabu hiyo itafute mastraika wenye uwezo mkubwa wa kufunga mabao, tofauti na sasa ambapo inabidi wasubiri dakika 90 ndipo washangilie.

Katika mechi tisa ambazo imeshinda, Yanga imeshinda mechi saba kwa bao 1-0.

Ni mechi mbili tu ambazo Yanga imeshinda zaidi ya bao moja. Mechi hizo ni dhidi ya Coastal Union iliposhinda mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Oktoba 3, mwaka huu na ule wa mabao 2-1 dhidi ya KMC, Oktoba 25 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Sare nne ambazo Yanga imetoka ni ya bao 1-1 dhidi ya Prisons, Simba na Namungo, huku ikitoka sare tasa dhidi ya Gwambina.

Makala haya yamekukusanya mechi saba ambazo Yanga imeshinda kwa bao 1-0, wakati huu ikiiusaka ubingwa...

**#1. Yanga 1-0 Mbeya City**

Yanga ilianza kupata ushindi wa bao 1-0 kwa mara ya kwanza Septemba 13, mwaka huu dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. Bao hilo likipatikana dakika tano kabla mechi kumalizika, likifungwa na Lamine Moro.

**#2. Kagera Sugar 0-1 Yanga**

Siku sita baadaye, Septemba 19, ikiwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Yanga ilipata tena ushindi wa bao 1-0. Lilikuwa ni bao lililofungwa na Mkongomani Mukoko Tonombe dakika ya 72 na kuipatia timu hiyo pointi tatu muhimu.

**#3. Mtibwa Sugar 0-1 Yanga**

Yanga iliendelea kuangusha moja moja, kwani Septemba 27, mwaka huu, ilitua kwenye Uwanja wa Jamhuri na kutoa kipigo cha bao 1-0, lililowekwa wavuni na beki Mghana Lamine Moro dakika ya 61 na kuifanya timu hiyo kuondoka na ushindi.

**#4. Yanga 1-0 Polisi Tanzania**

Ilikuwa ni Oktoba 22, mwaka huu, Mukoko Tonombe aliifungia Yanga bao pekee, ikishinda 1-0 dakika ya 69 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**#5. Biashara United 0-1 Yanga**

Michael Sarpong naye aliifungia Yanga bao pekee kwenye dakika ya 68 kwenye mechi iliyochezwa Oktoba 31, mwaka huu. Ni mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

**#6. Azam 0-1 Yanga**

Novemba 25, mwaka huu, Yanga ilipata ushindi wa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Azam Copmlex. Iliwachapa wenyeji Azam FC bao 1-0, lililowekwa wavuni na Deus Kaseke kwenye dakika ya 48.

**#7. Yanga 1-0 JKT Tanzania**

Kaseke tena kwa mara nyingine, aliifungia Yanga bao pekee kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ikishinda 1-0 dhidi ya JKT Tanzania. Ilikuwa ni dakika ya 48, likadumu hadi mwisho wa mchezo, ikiwa na mechi ya saba kushinda bao 1-0.

**JE, WAJUA?**



DIOGO Jota sasa amefikisha mabao tisa katika mechi 14 alizoichezea Liverpool, lakini akicheka na nyavu mara nane katika mechi nane zilizopita.





# Hospitali za rufani zaelekezwa ubunifu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Profesa Mabula Mchembe, amezishauri hospitali za rufani nchini kuwa wabunifu wa kutengeneza vifaa mbalimbali vya kutolea huduma za afya kwa jamii kama walivyofanya wakati wa mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid -19, ili kuepusha gharama za uagizaji nje.

Prof. Mchembe aliyasema hayo juzi, katika maadhimisho ya miaka 100 tangu kuanzishwa kwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Alisema kuna haja ya hospitali zote kuwa na ubunifu wa kutengeneza vifaa ambavyo nchi imekuwa ikitumia fedha nyingi kuviagiza nje ya nchi, ilhali kuna wataalamu wenye vipaji na ujuzi mkubwa wa kutengeneza vifaa hivyo.

"Naomba tujenge tabia ya kutumia vipaji vya wataalamu wa kutengeneza vifaa kama wapo, hatupaswi kubweteka kusubiri kila vifaa kutoka nje hata vile ambavyo uwezo wa kuvitengeneza upo," alisema Prof. Mchembe.

Alisema kipindi taifa liko kwenye mapambano ya ugonjwa wa corona, taasisi zikiwamo hospitali walijitahidi kutengeneza vifaa vya kujikinga na ugonjwa huo kama barakoa, vitakasa mikono na makoti, ambavyo vilisaidia katika utoaji huduma, hivyo kuna umuhimu wa kuendeleza utaratibu huo.

Alisema ni vyema utaratibu huo ukaendelezwa ikiwamo kila hospitali kuwa na kitengo cha kutengeneza vifaa vya utoaji huduma ya afya, ili vinapohitajika wagonjwa wasipate tabu ya kwenda kutafuta nje ya eneo wanalopatia huduma.

Katika hatua nyingine, aliwataka wafanyakazi kujenga tabia ya kufanya kazi kwa upendo, kusaidiana, kuelekezana, kujifunza na kushirikiana kwa watu wote bila kujali vyeo walivyonavyo, jambo litakalosaidia kutoa huduma bora kwa wananchi.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Ernest Ibenzi, alisema tangu kuanzishwa kwa hospitali hiyo kupitia serikali na waasisi mbalimbali waliopita, ambao walijitahidi kufanya kazi kubwa ya kuboresha miundombinu, bado kuna upungufu wa watumishi na majengo.

Kutokana na hilo, ameiomba serikali iendelee kutoa kipaumbele katika sekta ya afya kwa kuboresha miundombinu ili watumishi wafanye kazi kwa viwango vya hali ya juu.

Aliipongeza serikali kutokana na jitihada za kuboresha sekta ya afya hapa nchini kwa kujenga hospitali, vituo vya afya na zahanati katika maeneo mbal-



Mkuu wa Kitengo cha Kodi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Denis Masami, akitoa maelezo kwa wataalamu wa sekta ya ardhi katika ofisi ya Mtendaji Kata Chidachi kabla ya kuanza zoezi la kupita nyumba kwa nyumba katika mtaa wa Chidachi, jijini Dodoma, kuhamasisha ulipaji kodi ya pango la ardhi mwishoni mwa wiki. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# CKHT yatoa mafunzo elekezi kwa wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

CHUO Kikuu Huria cha Tanzania (CKHT) kituo cha Dodoma kimeendesha mafunzo elekezi kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea ikiwa ni sehemu ya kuashiria kuanza kwa mwaka mpya wa masomo wa 2020/21.

Mkurugenzi wa Kituo cha Mkoa wa Dodoma (CKHT), Dk. Seleman Ismail, alisema utaratibu wa OUT unatumia mikoa kama sehemu za kwanza kwa wanafunzi kupata huduma za kielimu mahali walipo.

"Siyo lazima upate kila huduma kwenye kituo cha mkoa kwa kuwa kuna baadhi ya huduma zinapatikana Makao makuu, hapa utaleta na tutaziwasilisha ili zifanyiwe kazi," alisema Dk. Ismail.

Alisema CKHT imejizatiti katika utoaji wa huduma ya elimu, hivyo wanafunzi wakitumie ili kupata elimu na kutimiza ndoto zao.

Akitoa maelezo katika mafunzo elekezi kituoni hapo, Dk. Anna Wawa, alisema CKHT inatumia mifumo ya teknolojia ya habari (TEHAMA) kutoa elimu hivyo bado hakuna namna ya kuikimbia teknolojia.

"Kwa mifumo ya ujifunzaji na ufundishaji wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kumiliki simu au kompyuta sio ufahari bali ni kitu cha msingi sana," alisema Dk. Wawa.

Kwa upande wake, Kiongozi wa Serikali ya Wanafunzi, Ismail Mussa, alisema CKHT ni taasisi ya umma ambayo inatoa elimu kama vyuo vingine japo kunaweza kuwa na utofauti katika mifumo ya ufundishaji na ujifunzaji.

Alisisitiza umuhimu wa wanafunzi kushirikiana kwa kuwa inasaidia kuwa na mtandao unaorahisisha wanafunzi kusaidiana katika masuala ya kitaaluma.

Mafunzo elekezi katika kituo cha Mkoa cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Dodoma yamehudhuriwa na wafanyakazi wa chuo hicho, wanafunzi wa mkoa wa Dodoma na wilaya zake na baadhi nje ya mkoa huo.

## Watoto 800 wajua kusoma, kuhesabu ndani ya siku 60

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANAFUNZI 809 kutoka shule za msingi tano za Wilaya ya Chamwino, wamejua kusoma na kuhesabu ndani ya siku 60.

Wamepata ufahamu huo kupitia mradi wa Jifunze unaotekelezwa katika shule hizo na Shirika la Uwezo Tanzania kwa kushirikiana na Women Wakeup (WOWAP).

Idadi hiyo ni sawa na asilimia 85 ya wanafunzi wa darasa la tatu mpaka la sita waliokuwa wakifundishwa kupitia mradi huo wa Jifunze, chini ya walimu wa shule hizo, ambao wamepata mafunzo na mbinu ya kuwafundisha wanafunzi wasiojua kusoma na kuhesabu.

Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamoga, alibainisha hayo juzi kwenye mkutano uliofanyika jijini hapa wa kutoa tathmini ya mradi wa Jifunze unaotekelezwa na Shirika la Uwezo Tanzania kwa kushirikiana na WOWAP katika shule hizo.

Nyamoga alisema mashirika hayo yanastaili pongezi kubwa sana, kwa sababu wamefanya jambo la msingi ambalo limetoa matokeo chanya ndani ya siku 60, kwa kufanikiwa kufuta ujinga kwa wanafunzi hao ambao wengi wao walishakata tamaa.

"Nawapongeza sana mashirika haya kwa kuleta mradi huo, lakini nawapongeza walimu waliopata mafunzo ya kuwafundisha wanafunzi hao wamefanya kazi kubwa," alisema Nyamoga.

Hata hivyo Mkuu huyo wa Wilaya aliwaagiza walimu waliopata mafunzo ya mbinu ya kumfundisha mwanafunzi asiyejua kusoma kuendelea na zoezi hilo kwa wanafunzi ambao waliachwa nyuma wakati wa utekelezaji wa mradi huo, ili kupunguza au kutokomeza idadi ya wasiojua kusoma na kuhesabu.

"Naomba walimu msibweteke kwa sababu mradi wa Jifunze umefikia mwisho, mnapaswa kuendelea kuwafundisha wanafunzi kwa sababu mbinu za mafunzo mnazo, ujuzi mnao hakuna sababu ya nyie kuacha kuwafundisha," alisema Nyamoga. Alisema wanapaswa kuendelea na madarasa hayo kwa vipindi ambavyo vimepangwa mkiwa na lengo moja la kuhakikisha mnafuta ujinga katika Wilaya ya Chamwino. Naye Mkurugenzi wa Uwezo Tanzania, Zaida Mgalla, alisema hakuna sababu ya shule hizo kuacha kufundisha wanafunzi waliopo katika shule hizo wakati vifaa wanavyo na elimu ya ufundishaji wanayo.

Mgalla alibainisha kuwa mbinu za kumfundisha mwanafunzi mpaka aelewe wanazo kazi iliobaki ni kuendeleza zoezi hilo, ili kuhakikisha shule hizo zinakuwa bora na kukosa wanafunzi wasiojua kusoma na kuhesabu.

Alisema mwalimu siku zote anapaswa kuwa mbunifu, hivyo wajenge utaratibu wa kufuatilia kwa karibu na kubuni mbinu ya nini kifanyike.

Awali Mkurugenzi wa WOWAP, Fatma Toufique, alisema iko sababu ya kuboresha mazingira ya mradi wa Jifunze katika shule nyingine kwa sababu huu wa awali umeleta matokeo chanya katika shule ambazo mradi umetekelezwa.

Alisema endapo shule zote zitafikiwa na mradi huo, basi Chamwino itakuwa mfano wa kuigwa na shule zote za mkoani Dodoma kutokana na kampeni za kufuta ujinga kupitia mradi wa Jifunze.





## 12 watiwa mbaroni tuhuma za uhalifu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia vijana 12 wakazi wa maeneo mbalimbali jijini hapa kwa tuhuma mbalimbali zikiwamo za kuvunja nyumba za watu na kuiba mali pamoja na kushiriki kwenye wizi wa vyombo vya moto.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, aliwambia waandishi wa habari juzi katika Kituo Kikuu cha Polisi cha Mbeya kuwa vijana hao walikamatwa wakati wa msako uliofanywa na kikosi maalumu cha jeshi hilo.

Kamanda Matei alisema katika tukio la kwanza jeshi hilo liliwakamata vijana sita ambao ni Raison Mwenga (26) Mkazi wa Iyela, Victor Mwashigale (38) mkazi wa Makunguru, Beatus Andrea (28) mkazi wa Uyole na Daud Mwang'ita (20) mkazi wa Iganzo jijini hapo.

Aliwataja wengine ni James Charles (27) na Thomas Andrea (22) wote wakazi wa Uwanja wa Ndege wa zamani ambao wote wanatuhumiwa kufanya matukio mbalimbali ya kuvunja nyumba za watu nyakati za usiku na kuiba, kuiba pikipiki na bajaji.

Alisema watuhumiwa walipopekuliwa walikutwa na mali mbalimbali za wizi zikiwamo Tv, radio, baiskeli, magodoro, mablanketi, meza za TV, kompyuta, majiko ya gesi, jiko la kupikia, mabegi ya nguo na sukari kilo 11.

Kamanda Matei alisema watuhumiwa hao walikiri kuiba bajaji moja yenye namba za usajili MC 747 CMV aina ya TVS ambayo ilikuwa imepotea katika maeneo ya Mianzini Mwakibete na kwenda kuificha Iganzo ambako ni zaidi ya kilomita 10 kutoka walipoiiba.

"Hawa vijana wamekuwa wakitusumbua sana, wakiingia nyumbani kwako wanapita na chochote wanachokikuta, lakini sasa wameshanaswa na tunatarajia kuwafikisha mahakamani upelelezi utakapokuwa umekamilika," alisema Kamanda Matei.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linawashikilia vijana wengine sita wote wakazi wa Isanga jijini hapa kwa tuhuma za kukutwa na dawa za kulevya aina ya bhangi wakitumia na kuuza.

Aliwataja vijana hao ni Nosha Ndomba (27), Meshack Toto (19), Alex Mwaliyoyo (25), Juma White (18), Mustafa White (22) na Ally White (24) ambao walikutwa na kete 30 ambazo ni sawa na uzito wa gram 150.

Alisema vijana hao walikamatwa Novemba 25, mwaka huu saa 2:00 usiku katika eneo la Ilolo lililopo Kata ya Sinde jijini hapa huku akidai kuwa vijana hao pia huwa wanajihusisha na matukio ya wizi.

# Jiji lashtukia njama za kutapeliwa mil. 108/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imenusurika kupoteza zaidi ya Sh. milioni 108 baada ya wazee sita wakazi wa Mtaa wa Ikuti Kata ya Iyunga jijini hapa kudaiwa kuwasilisha madai ya uongo wakitaka walipwe kiwango hicho cha fedha kama fidia ya eneo la Soko la Ikuti wakidai ni la kwao.

Kutokana na madai hayo, uongozi wa halmashauri ulishaanza kuingia mkenge kwa kuwalipa shilingi milioni 17 kabla ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuwashtukia na kuagiza Jeshi la Polisi kuwatiwa mbaroni.

Wazee hao waliotaka kulipwa fedha hizo ni Aron Mwalyembesi, Andrew Mwakijengele, James Mwaidafu, Richard Mwaibeju, Ndiga Mwanjela na Mwashoroji Kwesu ambao wote ni wakazi wa Mtaa wa Ikuti na wote wana umri wa zaidi ya miaka 60.

Chalamila alifika katika eneo hilo juzi akiwa ameongozana na baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa lengo la kutatua mgogoro huo, uliodumu muda mrefu na ndipo akaamua kusikiliza pande zote mbili.

Mmoja wa wazee hao, Aron Mwalyembesi, alisema eneo hilo walikuwa wanalimiliki tangu miaka ya 1970 na walikuwa wanalitumia kama eneo la klabu ya umoja wa wazee ambao walikuwa zaidi ya 70 na walijenga nyumba sita kwa ajili ya kunywea pombe za kienyeji.

Alisema kadri muda ulivyokuwa unaenda wanachama walikuwa wanapungua kutokana na baadhi kuacha kunywa pombe na kuanza kusali, baadhi walifariki na wengine walihama katika eneo hilo na kwenda katika maeneo mengine.

"Hili eneo tunalimiliki kihalali na tunazo nyaraka na vielelezo vyote vinavyoonyesha kwamba sisi tunaidai halmashauri fidia, huu mgogoro tulianza nao mbali sana na tunaendelea kudai," alisema Mwalyembesi.

Akitolea ufafanuzi wa mgogoro huo, Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, alisema wazee hao walifika ofisini kwake wakitaka kulipwa fidia hizo na ndipo akaamua kuanza kufuatilia ili kujua uhalali wa malipo hayo.

Alisema baada ya kupitia nyaraka mbalimbali alibaini kuwa taarifa wanazozitoa wazee hao wanaodai kuwa eneo hilo walipewa wao sio za kweli na badala yake waliokuwa wanalitumia ni wazazi wao ambao kwa sasa hawapo hai.

Hata hivyo, alisema wazee hao wameidanganya serikali kwa kuorodhesha majina ya marehemu na kugushi saini zao ili kutimiza idadi ya watu 15 ambao wanadai.

"Hii inaonyesha wazi kuwa madai ya wazee hawa hayajasimama kwenye misingi ya ukweli, hivyo hata hizo fedha ambazo walishalipwa walilipwa kimakosa na hawakuwa wanastahili kulipwa hata kidogo," alisema Ng'wanidako.

Naye Chifu wa kabila la Wasafwa wa eneo hilo, Nelson Mhena, alisema wazee hao walipewa eneo hilo bure na aliyekuwa chifu wa wakati huo, lakini sio soko lote kama wanavyodai wao na badala yake kulikuwa na mabanda yao ambayo yalikuwa sita.

Baada ya maelezo hayo, Chalamila aliliamuru Jeshi la Polisi kuwakamata wazee hao na kuwasweka ndani, huku akimtaka Mwanasheria wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuhakikisha wanafikishwa mahakamani.

"OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), Kamata hawa peleka ndani wakae huko, hatuwezi kuvumilia 'upumbavu' kama huu, mwanasheria hakikisha hawa wanapelekwa mahakamani Jumatatu," aliagiza Chalamila.

Baada ya Chalamila kutoa maagizo hayo, aaskari waliwasaka wazee hao kwenye mkutano na kuwanasa wote kisha wakaondoka nao kwenda Kituo Kikuu cha Polisi cha Mbeya.



Baadhi ya wahitimu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Ndaki ya Mbeya, wakiwa wamevalia majoho mwishoni mwa wiki wakati wa sherehe za kutunukiwa shahada mbalimbali na Mkuu wa Chuo hicho, anayemaliza muda wake, Jaji Mkuu mstaafu, Barnabas Samatta. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Miundombinu ya chuo kikuu kukarabatiwa kwa bil. 15/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetumia zaidi ya Sh. bilioni 15 kujenga na kukarabati miundombinu mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Miundombinu hiyo ni kumbi za mihadhara na mabweni ya wanafunzi ndani ya miaka mitano, hivyo kukifanya chuo hicho kuwa miongoni mwa taasisi zenye miundombinu bora.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Lugano Kusiluka, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 19 ya chuo hicho, Ndaki ya Mbeya ambapo alisema uwekezaji huo haujawahi kutokea tangu chuo hicho kilipoanzishwa.

Alisema ujenzi wa miundombinu hiyo umesaidia kuboresha mazingira ya wanafunzi wa chuo hicho kujifunzia na kuishi, huku akiwaomba wadau kuendelea kuchangia ujenzi wa miundombinu inayohitajika.

Prof. Kusiluka alisema pamoja na ujenzi wa uwekezaji huo uliofanywa na serikali, lakini chuo hicho Ndaki ya Mbeya kinakabiliwa na uhaba wa hosteli za wanafunzi pamoja na makazi kwa ajili ya wafanyakazi. Alisema chuo hicho kina eneo kubwa katika Kata ya Iwambi jijini Mbeya ambalo limeshafanyiwa mpango wa matumizi na miongoni mwa miundombinu inayokusudiwa kujengwa ni hosteli na makazi ya watumishi.

"Tunawaalika wawekezaji mbalimbali kuja kuwekeza kwenye eneo hilo, Baraza la Chuo limeshapitisha sera ya uwekezaji na linafaa kwa ajili ya miundombinu mbalimbali," alisema Prof. Kusiluka.

Mwenyekiti wa Baraza la chuo hicho, Prof. Mathew Luhanga, alishukuru serikali kwa kuidhinisha fedha hizo, huku akimpongeza Rais, Dk. John Magufuli kwa ujasili aliouonyesha kwenye mapambano ya janga la virusi vya corona.

Alisema endapo Rais Magufuli asingekuwa jasiri, janga hilo lingekuwa linaendelea mpaka sasa kama ilivyo katika mataifa mbalimbali ambayo yamefunga shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo mikusanyiko ya sherehe.

Aliwataka wahitimu wa chuo hicho kuiunga mkono serikali kwa kufanya kazi kwa bidii kwa maelezo kuwa wengi wao wamesoma kwa mkopo wa serikali uliokuwa unatolewa kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELSEB).

Aliwataka kuisaidia serikali kufikia mapinduzi ya nne ya viwanda kwa kufanya utafiti mbalimbali zinazohusiana na maendeleo ya sekta hiyo pamoja na kutunza takwimu ambazo alidai ndiyo rasilimali muhimu zaidi.

"Lakini nawaomba msiridhike na elimu mliyopata na badala yake mjiendeleze na muisaidie serikali kutunza vizuri takwimu kwa kutumia teknolojia za kisasa vinginevyo tutaachwa na mataifa mengine kwenye mapinduzi haya ya nne kama tulivyoachwa na yale ya awali," alisema.

Mkuu wa Chuo hicho Ndaki ya Mbeya, Prof. George Shumbusho, aliwataka wahitimu wa chuo hicho ambao wamefaulu vizuri kutovimba vichwa na wale waliofeli wasikate tamaa.





Viongozi wa CCM Tawi la Shangani, wakimjulia hali Nasra Mohamed Abdallah (KARUME) (72), ambaye anaumwa nyumbani kwake Migombani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Watendaji wanaovuruga kesi za udhalilishaji wamkera DC

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Chakechake Pemba, Rashid Khadid Rashid, amesema haridhishwi na utendaji kazi wa baadhi ya watendaji wa mahakama, polisi pamoja na wanaharakati wanaoshiriki kufanya suluhu dhidi ya kesi za udhalilishaji.

Alisema hali hiyo inachangia kukwamisha juhudi za serikali za kutokomeza vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto kisiwani humo.

Aliyasema hayo wakati akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia katika viwanja wa Gombani Kisiwani Pemba yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) upande wa Zanzibar.

Mkuu huyo wa Wilaya alizitaka kamati za kupinga udhalilishaji kushirikiana na Ofisi ya Mufti kutoa elimu ya ndoa kwa wanandoa pamoja na sehemu zenye mikusanyiko ya watu zikiwamo shule.

Alisema kesi nyingi za udhalilishaji zinashindwa kupatiwa ufumbuzi wa haraka kutokana na kuwapo baadhi ya watumishi wa vyombo vinavyosimamia sheria kukosa uadilifu.

"Miongoni mwa mambo yanayochangia kesi hizi ziendelee kutokea ni uwapo wa baadhi ya watumishi ambao sio waadilifu wanaoshiriki kufanya suluhu, pamoja na hukumu ndogo zinazotolewa dhidi ya watuhumiwa," alisema. Akizungumzia kuhusu mwenendo wa matukio hayo Kisiwani Pemba, alisema bado tatizo hilo lipo kwa kiwango kikubwa katika jamii licha ya matukio hayo kuanza kupungua ikilinganishwa na miaka iliyopita ikiwa ni kutokana na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na wanaharakati mbalimbali ikiwamo TAMWA.

"Naomba niiambie hadhira hii kuwa vitendo vya udhalilishaji bado ni tatizo kubwa na matukio haya yanaripotiwa kila siku katika jamii zetu, kwa mwaka huu hadi sasa tuna kesi 218 ambazo zinafanyiwa kazi katika ngazi mbalimbali ambapo kwa Wilaya ya Wete ni 57, Micheweni 30, Chakechake 84, na Mkoani 47 ambapo kesi za ubakaji ndizo zinazoongoza kwa wingi katika kesi hizi," alisema.

Naye Mratibu wa TAMWA Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema lengo la kuandaliwa kwa mazoezi hayo ya hiari ya siku moja ni kubadilisha tabia hasa za vijana dhidi ya fikra potofu za kubaka na kudhalilisha kwa ujumla kupitia ufanyaji wa mazoezi.

"TAMWA Zanzibar kwa kuwa ni wadau wakubwa wa kupambana na udhalilishaji wa wanawake na watoto tumeamua kuadhimisha siku hii kwa kufanya mazoezi ya hiari ili kupaza sauti za wanyonge kupitia kampeni ya siku 16 za kuhamasisha jamii kubadili tabia juu ya ukatili wa mtoto wa kike," alisema.

Aidha, mratibu huyo alisema TAMWA itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali, ili kuhakikisha wanawake na watoto wanaishi bila ya ukatili na udhalilishaji. Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya Wanawake Pemba, Mwanaisha Ali Massoud, alisema siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto wa kike ni muhimu kwa jamii, ili kutafakari namna ya kuyakinga makundi hayo dhidi ya ukatili.

Alisema udhalilishaji na ukatili huathiri sana wanaofanyiwa ikiwamo kukatisha ndoto zao ziwe za kielimu au biashara kutokana na athari zake.

Alisema: "Njia rahisi ya kupambana na matendo hayo ni kwa jamii kuondoa muhali na kushirikiana na vyombo vya sheria ikiwamo Polisi na Mahakama." Tatu Abdallah Msellem kutoka Jumuiya ya Tumaini Jipya Pemba (TUJIPE) alitoa wito kwa taasisi na idara za serikali kuongeza ushirikiano na asasi za kiraia hasa suala la upatikanaji wa takwimu ili kufanikisha mapambano dhidi ya vitendo hivyo.

# Waziri azuia hati za matumizi ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi, Maendeleo na Makaazi, Riziki Pembe Juma, amezuia hati ya matumizi ya ardhi kwa baadhi ya maeneo ya Unguja na Pemba zilizotolewa miezi miwili kabla ya uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Akizungumza jana katika eneo la Tunguu Mkoa wa Kusini Unguja, alisema serikali imezuia maeneo hayo yaliyotolewa kati-ka kipindi miezi miwili kabla ya uchaguzi wa Oktoba na kuwataka wananchi waliopewa hati na kupimiwa maeneo kuripoti kwa wakuu wa wilaya wa maeneo yao.

Alisema hatua hiyo ni miongoni mwa maagizo ya Rais wa Zanzibar na itasaidia kujua maeneo hayo kama yametolewa kwa mujibu wa sheria na taratibu za ardhi.

"Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, baada ya kuwaapisha mawaziri aliowateua akiwamo mimi alisema kabla ya uchaguzi kuna maeneo ya ardhi yametolewa bila ya kufuata utaratibu na kuagiza kuwa apelekewe ripoti kuhusu maeneo hayo ya ardhi yaliyotolewa," alisema waziri huyo.

Pembe alisitisha hati ya matumizi ya ardhi katika eneo la Tunguu na kusimamisha shughuli za ujenzi wa mgahawa uliojengwa kinyume cha taratibu karibu na maeneo ya Ofisi za Serikali huko Tunguu Wilaya ya Kati Unguja.

Aliwataka wananchi kufuata sheria na taratibu za matumizi ya ardhi ili kuepukana na migogoro ya ardhi ambayo inaweza kujitokeza.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, aliziomba mamlaka za usimamizi wa ardhi kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali kabla ya kutoka kibali cha matumizi ya ardhi kwa jamii ili kuepusha hasara pamoja na migogoro inayoweza kujitokeza.

# Bohari Kuu yaagizwa upatikanaji wa dawa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Bohari Kuu Zanzibar ametakiwa kuharakisha upatikanaji wa dawa katika Bohari Kuu ya Pemba, ili kuepuka upungufu wa dawa zinazohitajika kwa wananchi wanaofuata huduma za afya katika hospitali na vituo vya afya kisiwani Pemba.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na uongozi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii baada ya kufanya ziara maalum ya kuangalia upatikanaji wa huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Hemed alishuhudia upungufu wa baadhi ya dawa ndani ya ghala ya hospitali hiyo ambazo kwenye ghala kuu zipo na kusema iwapo kuna tatizo katika mfumo wa mtandao wa usambazaji dawa kati ya Bohari Kuu na hospitali washirika lazima litafutiwe ufumbuzi wa haraka ili kuondosha usumbufu unaoweza kuwaathiri wananchi.

Alisema haipendezi kuona hitilafu nyingi zilizojichomoza kwa kipindi kifupi na kuleta changamoto katika utendaji kazi katika maeneo mengi ya huduma baadhi ya viongozi na watendaji husingizia uwapo wa corona ambayo imeisumbua jamii kwa miezi sita wakati matatizo mengine yana zaidi ya mwaka sasa.

Makamu wa Pili wa Rais aliuhimiza uongozi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuandaa utaratibu wa kuwaajiri vijana wataalamu waliopata mafunzo mbalimbali ya fani ya afya ili kujaza mapungufu yaliyomo ndani ya hospitali na vituo vya afya nchini.

Alisema yapo maeneo kadhaa ya huduma za afya katika baadhi ya hospitali yaliyokosa watendaji akitolea mfano vitengo vya maabara, upasuaji na hata huduma za mama na mtoto wakati vijana wenye taalum hiyo wameachwa na kuzagaa mitaani.

"Wale waliosomeshwa na tayari wamefanikiwa kuwa na taaluma ya kutosha ni vyema wakatafutiwa utaratibu wa kuajiriwa badala ya kuachwa wakaendelea kuzurura mitaani na matokeo yake hujiingiza katika vitendo visivyokubalika," alisema Hemed.

Akizungumzia madeni na haki za watendaji wa afya, alisema uongozi wa Wizara ya Afya lazima ujipange vyema katika kuona masuala hayo muhimu yanapatiwa ufumbuzi wa haraka.

Naye Daktari Dhama wa Hospitali ya Wilaya ya Micheweni, Dk. Mbwana Hamad Shoka, alisema upatikanaji wa huduma za mama na mtoto kwenye hospitali hiyo zinaendelea kuimarika na kusananisha vifo vya mama na mtoto kupungua.

Alisema bado upo upungufu wa wauguzi wa kusimamia huduma hizo kutokana na ongezeko la kinamama wanaohitaji huduma hizo muhimu zinazopaswa kuwa na uangalifu wa hali ya juu.

# Mpango: Uhaba wataalamu unaikosesha serikali mapato

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amesema kuwa uhaba wa wataalamu wa masuala ya kodi, umekuwa unaikosesha serikali mapato.

Amesema Chuo cha Kodi (ITA) kifanye utafiti na kuwapa mbinu bora wahitimu wake, ili kukuza mapato.

Pia,alikitaka chuo hicho, kufanya utafiti zaid ili kupata mbinu bora zaidi za ukusanyaji kodi hususani kodi ya majengo.

Aliyasema hayo katika mahafali ya 13 ya chuo hicho, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, katika hotuba yake iliyosomwa na Kamishna wa Sera za Ununuzi wa Umma kutoka wizara hiyo, Dk. Fredrick Mwakibinga.

"Mfumo wa kodi ili uwe sahihi unahitaji watalaamu hawa, kunamabadiliko makubwa katika sekta hii, ITA iangalie namna ya kuboresha mifumo ya kodi ya majengo, kupitia utafiti," alisema.

Alisema serikali imekuwa ikipoteza fedha za kodi na kwamba wataalamu hao kupitia utafiti, watasaidia kutoa ushauri wa namna ya kukusanya kodi.

Dk. Mpango alisema uzoefu unaonyesha kuwa serikali imekuwa ikipoteza mapato kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo, ukwepaji kodi.

"Chuo hiki kipitie mtaala wake ili wahitimu waweze kukabiliana na ushindani sokoni na masuala ya kufanikisha ukusanyaji wa kodi," alisema Waziri Mpango.

"Kituo hiki kwa kushirikiana na wadau tunataka kiwe kituo cha umahiri." Mkuu wa chuo hicho, Prof. Isaya Jairo, alisema tangu mwaka 2008 wamekwishatoa mafunzo kwa wahitimu 12,000 sawa na asilimia 83.

Prof. Jairo alisema chuo hicho kinatarajia kuanzisha mafunzo ya masafa ya mbali kwa kutumia mtandao, ili kutoa fursa kwa wanaohitaji elimu ya kodi, ushuru na mapato.

"Katika matokeo ya utafiti wetu mafunzo kwa wahitimu hawa wakiyatumia ipasavyo, yatafanikisha ukusanyaji kodi na mapato kuongezeka (TRA)," alisema Prof. Jairo.

Pia alieleza kuwa chuo hicho, kimekuwa kikitoa mafunzo kwa wanafunzi kutoka nchi mbalimbaliza Kusini mwa Afrika na ukanda wa Afrika Mashariki, na kwamba kiliteuliwa kuwa kituo umahiri kuhusu masuala ya ushuru na kodi kwa ukanda huo.

"Chuo kimesaini makubaliano na nchi ya Sudan Kusini, kutengeneza mpango kazi wa ushuru, kodi na mapato katika mamlaka ya nchi yao," alisema Prof. Jairo.

Jumla ya wahitimu 389 walitunukiwa vyeti katika ngazi ya shahada, stashahada na astashahada.




Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS, Casmir Kyuki, akizungumza na wawekezaji mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa mikutano ya mwaka wa mifuko ya uwekezaji ya pamoja inayoendeshwa na UTT AMIS, kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Simon Migangala, na mjumbe wa bodi hiyo, Fransis Chacha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataka mabadiliko mtaala VETA

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeombwa kufanya mabadiliko ya mtaala wa vyuo vya Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ili uendane na uhalisia wa mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Imeelezwa kuwa hatua hiyo itakayowezesha wahitimu wake kuisaidia nchi kukuza sekta ya viwanda.

Wakitoa ombi la mabadiliko hayo, wahitimu wa chuo cha VETA Kigoma wakati wa mahafali yao, walieleza kuwa wahitimu kutoka katika vyuo vya mamlaka hiyo, wanapaswa kuandaliwa ili kukidhi kutumika katika kipindi hiki cha mabadiliko ya teknolojia.

Mmoja wa wahitimu hao, Aron Elias, alisema teknolojia inayotumika katika baadhi ya fani ikiwamo kompyuta na ufundi bomba, ni ya zamani tofauti na uhalisia wa soko la ajira ambalo linatumia mfumo wa kisasa.

Benita Bahina mhitimu wa fani ya ufundi bomba, alisema jamii inapaswa kuwapokea vyema na kuwatumia mafundi waliopitia VETA na kuachana na mawazo potofu juu yao, kwani elimu walioipata kwa kiasi kikubwa ina manufaa kwa jamii.

Naye Kaimu Mkuu wa Chuo cha VETA Kigoma, Sirili Aloyce, alieleza kupitia mtaala uliopo, wanawaandaa wahitimu vyema kuajiriwa, na kuajiri kupitia fani mbalimbali walizosomea, hatua itakayowezesha kupunguza wimbi la vijana wasio na ajira.

Pia, alieleza kuwa kulingana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia, mtaala wa mafunzo hayo unapaswa kupitiwa mara kwa mara na kufanyiwa mabadiliko kwani fursa mbalimbali zinazotokea nchini zinahitaji mfundi waliofundishwa kutumia teknolojia hizo.

Ofisa Maendeleo ya Vijana Manispaa ya Kigoma /Ujiji, Ramadhani Masale, aliwataka wahitimu hao kuungana na kuanzisha vikundi vya kufanya kazi ili kukopesheka na kupata fedha zinazotolewa na halmashauri kwa makundi ya vijana.

# Wananchi wapewa uhakika utekelezaji miradi yote ya maji

**Na Neema Hussein, SONGEA**

SERIKALI imesema ina fedha za kutosha kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maji kwenye maeneo mbalimbali nchini, ukiwa ni mkakati wa kumaliza kero ya maji kwa wananchi.

Kauli hiyo ya serikali imetolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizaya ya Maji, Mhandisi Anthny Sanga, baada ya kukagua ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji cha Litisha wilayani Songea unaotekelezwa na wakala wa Maji Vijijini RUWASA na kujengwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Songea (SOUWASA).

Aidha, Sanga aliwahakikishia wananchi wa Jimbo la Peramiho Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma kuwa tatizo ya maji linalowakabili wananchi wa jimbo hilo litakwisha katika kipindi cha miezi miwili kuanzia sasa.

Sanga aliahidi kutoa Sh. milioni 200 wiki ijayo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa maji katika kijiji hicho ambao ujenzi wake umefikia asilimia 85.

Alisema mradi huo utakamilika haraka iwezekavyo ili wananchi wa Litisha waweze kupata maji kwani wamechoka kusubiri huduma hiyo kwa muda mrefu.

Sanga aliwataka watendaji wa Wizara ya Maji kuhakikisha wanatekeleza miradi ya maji kwa weledi na kujiepusha na vitendo vinavyoweza kukwamisha juhudi zinazofanywa na serikali zinazolenga kuboresha maisha ya Watanzania.

Pia, aliwaagiza wataalamu hao kuanza mchakato wa kuwaunganishia maji wananchi wa kijiji hicho, majumbani kwani ndani ya siku 60 mradi utakamilika, hivyo siyo vyema wasubiri hadi maji yatakapoanza.

Awali, Mbunge wa Peramiho, Jenista Mhagama, aliishukuru serikali kwa usimamizi na utekelezaji mzuri wa miradi ya maji katika vijiji mbalimbali katika jimbo hilo, na kuiomba wizara kukamilisha baadhi ya miradi ambayo bado haijakamilika.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Menas Komba, alimshukuru Katibu Mkuu kwa uamuzi wake wa kufika jimbo la Peramiho kuangalia utekelezaji wa miradi ya maji na kuahidi kuwa, miradi hiyo itatunzwa ili iweze kudumu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

## HABARI KIMATAIFA

# Jeshi la Ethiopia laikomboa Mekelle

**Addis Ababa,** Ethiopia

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Ably Ahmed, amesema majeshi ya nchi hiyo yamechukua udhibiti wa mji mkuu wa Jimbo la Tigray, Mekelle.

Ably alitangaza kuwa serikali ya shirikisho sasa imechukua udhibiti kamili wa mji huo, ikiwamo uwanja wa ndege, taasisi za umma, ofisi za utawala wa jimbo hilo na maeneo mengine muhimu.

Katika ujumbe wake kupitia ukurasa wake wa Twitter Jumamosi, Ably alitangaza pia kuwa wamemaliza operesheni yao ya kijeshi katika jimbo hilo.

Alisema maelfu ya wanajeshi ambao walikamatwa na wapiganaji wa chama tawala katika jimbo hilo, 'Tigray People's Liberation Front'- TPLF, yaani Chama cha Ukombozi wa Watigray pia wameachiliwa huru.

**Serikali ya Ethiopia ilianzisha mashambulizi ya kijeshi dhidi ya TPLF zaidi ya wiki tatu zilizopita kwa lengo la kuwaondoa madarakani.**

Chama cha TPLF kimekuwa madarakani katika jimbo hilo la kaskazini mwa Ethiopia.

Serikali ya Ethiopia ilianzisha mashambulizi ya kijeshi dhidi ya TPLF zaidi ya wiki tatu zilizopita kwa lengo la kuwaondoa madarakani.

Awali, ripoti katika shirika la habari linalohusishwa na serikali ya jimbo hilo zilisema mji wa Mekelle ulishambuliwa kwa makombora mazito.

Hata hivyo, jopo kazi lililoundwa na serikali kuu kufuatilia mzozo wa Tigray, limesema hayo ni madai ya uwongo ambayo yanaenezwa na TPLF, kwamba serikali kuu imefanya mashambulizi dhidi ya miji na maeneo ya makaazi ya raia.

Kulingana na taarifa ya serikali kuu, vikosi vya serikali vinalenga tu maghala ya silaha za kijeshi ya TPLF, pia wanajeshi wa serikali ya shirikisho hawajafanya mashambulizi yoyote dhidi ya miundombinu muhimu ya raia kama hospitali, shule au maeneo ya makazi. Taarifa hiyo iliongeza kuwa wanajeshi wa vikosi vya serikali, havijafanya mashambulizi katika maeneo yenye watu wengi.

Mwishoni mwa wiki, mkuu wa majeshi wa Ethiopia, Jenerali Berhanu Jula, alisema baada ya vikosi vyake kuchukua udhibiti kamili wa mji wa Mekelle, sasa wanawasaka wapiganaji wa TPLF wanakojificha.

Machafuko ya Jimbo la Tigray yalianza mapema mwezi huu, wakati Waziri Mkuu wa Ethiopia, Ably Ahmed ambaye pia ni mshindi wa tuzo ya Amani ya Nobel mwaka 2019, alipoviamrisha vikosi vyake kuanza operesheni kwa lengo la kuuondoa uongozi wa Jimbo la Tigray.

Mamia ya watu wameripotiwa kuuawa na zaidi ya Waethiopia 40,000 wamekimbia vita na kuingia Sudan. **DW**

## Chanjo ya corona kusafirishwa Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

CHANJO dhidi ya covid-19 iliyozalishwa na Pfizer na BioNTech yaanza kusafirishwa Marekani.

Kampuni ya dawa ya Kimarekani ya Pfizer na kampuni ya bioteknolojia ya BioNTech iliyoanzishwa na mwanasayansi wa Kituruki Prof. Dk. Ugur Sahin (pichani) kutoka Ujerumani, inadaiwa kuanza kusafirishwa kwenda Marekani.

Kulingana na taarifa ya kituo cha biashara za ndani iliyochapishwa na gazeti la Wall Street Journal, iliarifiwa kwamba ndege za United Airlines zinatumiwa kusafirisha chanjo hiyo.

Katika taarifa hiyo, ilifahamishwa kwamba safari za kwanza zilitekelezwa kati ya Brussels na Chicago, ambapo chanjo hizo zitawasilishwa na baadaye kutolewa Chicago kwenda vituo vya usambazaji.



Taarifa zaidi zinaarifu kwamba Shirikisho la Usafiri wa Anga (FAA) limeidhinisha usafirishaji wa chanjo hizo ambazo zinapaswa kuhifadhiwa kwenye barafu kavu.

Pfizer na BioNTech, ambazo iliwasilisha ombi kwa Mamlaka ya Vyakula na Dawa ya Marekani (FDA) kwa matumizi ya dharura, tayari zilikuwa zimeanza kuomba taasisi za Ulaya.

Katika majaribio ya kliniki, maombi ya chanjo ya Pfizer na Biontech yalikuwa asilimia 95, chanjo ya Moderna asilimia 95.4, chanjo ya AstraZeneca na Oxford asilimia 70, ambapo zimekuwa na ufanisi asilimia 90 katika kila kipimo nusu na kizima cha dozi. **TRT**




Kimbunga Eta na Iota, kimeacha watu 150,000 bila makazi katika kitongoji cha Planeta baada ya Mto Chamelecón kuvunja kingo zake, nchini Honduras, jana. **PICHA: BBC**

# Boko Haram yashtumiwa kuua 40

**MAIDUGURI,** Nigeria

KUNDI la kiislamu la Boko Haram, limewaua takribani watu 40, ikiwamo wavuvi na wakulima wa mpunga wakati wakiendelea kuvuna Kaskazini mwa Borno, Nigeria.

Shambulio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki, eneo la Garin Kwashebe, Borno ambalo ni maarufu kwa kilimo hicho wakati wakazi wa hapo wakipigakura kwa mara ya kwanza tangu miaka 13 iliyopita, kuchagua mabaraza ya serikali za mitaa.

Malam Zabarmari, kiongozi wa jumuiya ya wakulima hao, Borno, alithibitisha kutokea tukio hilo akizungumza na vyombo vya habari.

"Wakulima walishambuliwa eneo la Garin-Kwashebe katika jamii hiyo na inakadiriwa watu 40 hadi 60, waliuawa," alisema kiongozi huyo.

Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari, alisema:

"Ninalaani mauaji ya wakulima wetu wanaofanya kazi kwa bidii baada ya kushambuliwa na magaidi katika Jimbo la Borno.

Nchi nzima imeumizwa na mauaji haya ya kipuuzi. Ninatuma salamu za rambirambi kwa familia na roho za marehemu zipumzike kwa amani," alisema katika taarifa yake. Rais Buhari alisema serikali imetoa msaada wote unaohitajika kwa vikosi vya jeshi ili kuchukua hatua zote muhimu.

Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Ahmed Satomi, anayewakilisha Jimbo la Jere eneo la Borno, alisema mazishi ya watu 44 yamefanyika jana.

Vyanzo vya habari eneo hilo, vilisema Boko Haram, wamekuwa wakiwashinikiza wanakijiji kulipa kodi kinyume cha sheria, kulipia mifugo na mazao. **AP**

## Bomu laua wanausalama 30

**KABUL,** Afghanistan

MLIPUKO wa gari nchini Afghanistan katika mji wa Ghazni umeua takribani watu 30.

Vyombo vya usalama na maofisa walisema kuwa inakadiriwa majeruhi wataongezeka kulingana na ukubwa wa tukio.

Mkurugenzi wa Hospitali eneo la Ghazni, Baz Mohammad Hemat, alisema miili 30 na majeruhi 24 walifikishwa hospitalini hapo.

"Waathirika wote ni wana usalama," alisema mkurugenzi huyo.

Shambulio lililenga kambi ya walinzi wa umma na vikosi vya usalama, maofisa walisema.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Tariq Arian, alithibitisha kuwa kulikuwa na gari ambalo lilisababisha mlipuko, bila kutoa maelezo zaidi.

**REUTERS**

# GUARDIOLA AMHAKIKISHA MAHREZ NAFASI KIKOSINI




**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola atataka "zaidi, zaidi na zaidi" kutoka kwa wachezaji wake baada ya Manchester City kuifumua Burnley mabao 5-0, huku akimsifia Riyad Mahrez kwa kufunga 'hat-trick'.

Benjamin Mendy na Ferran Torres pia walifunga kwa kikosi hicho cha Guardiola ambacho mwanzoni mwa miezi ya kwanza ya msimu huu kilikuwa na tatizo la kufunga.

Mabao hayo matatu ya Mahrez yalimfanya afikishe saba katika mechi nne zilizopita za Ligi Kuu dhidi ya Burnley.

Jumla ya mabao yote aliyowafunga Burnley kwenye Ligi Kuu yamefika nane na maana yake amewafunga mabao mengi zaidi kuliko timu nyingine yoyote kwenye Ligi Kuu England.

Raia huyo wa Algeria sasa amehusika katika mabao 102 kwenye Ligi Kuu (mabao 61, pasi za mwisho 41), na kumfanya kuwa mchezaji wa sita kutoka Afrika kufikisha idadi hiyo.

Na kiwango hicho cha Mahrez sasa kinaonekana kumuweka kwenye nafasi ya kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha Man City, huku Guardiola akisisitiza muda wa mzunguko wa wachezaji ndani ya kikosi hicho kwenye Ligi Kuu umemalizika, angalau hadi katika hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Februari.

"Bila shaka kutakuwa na wachezaji ambao wamechoka na wanahitaji kupumzika," alisema Guardiola.

# Neymar aweka rekodi ya mabao Ufaransa

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Neymar amefikisha mabao 50 kwa haraka zaidi kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, ikiwa ni rekodi kwa wachezaji wa karne hii.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil alifunga kwa penalti kwenye mchezo huo wa Jumamosi dhidi ya Bordeaux nyumbani wakati wakitoka sare ya mabao 2-2.

Neymar, ambaye wakati akijifua kabla ya mchezo huo, alivaa jezi yenye jina la Diego Maradona kwa ajili ya kutoa heshima kwa gwiji huyo aliyefariki wiki iliyopita, pia alikuwa na mchango katika bao la pili lililofungwa na Moise Kean.

Bao hilo la Neymar lilikuwa la 50 kwenye Ligi ya Ufaransa kuifungia PSG katika mechi 58 tangu alipojiunga na timu hiyo Agosti 2017 kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia ya euro milioni 222 kutoka kule Barcelona.

Mchezaji ambaye alikuwa anashikilia rekodi ya kufunga idadi ya mabao kama hayo kwa haraka zaidi tangu mwaka 2000 ni straika wa zamani wa PSG, Zlatan Ibrahimovic, ambaye alihitaji mechi 59 kufikisha idadi hiyo.

Radamel Falcao anashika nafasi ya tatu akiwa amefunga mabao 50 katika mechi 72, mbele ya Pauleta (mechi 75) na Kylian Mbappe (mechi 88).

Neymar mwenye umri wa miaka 28, ameshinda mataji nane tangu atue kwa miamba hao wa mji mkuu wa Ufaransa, yakiwamo mataji matatu mfululizo ya Ligi Kuu.

Bado hawajaweza kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na timu hiyo, ingawa PSG ilifika fainali kwa mara ya kwanza msimu uliopita na walifungwa na Bayern Munich bao 1-0.







# 'Pengo la Van Dijk halizibiki Liverpool'

**AMSTERDAM,** Uholanzi

ITAKUWA vigumu kwa Liverpool na Uholanzi kwa kuziba pengo la Virgil van Dijk kwa kipindi atakachokosekana dimbani kutokana na kuwa majeruhi, lakini hiyo haimaanishi kwamba, hawawezi kushindana, kwa mujibu wa gwiji, Clarence Seedorf.

Van Dijk aliumia goti mwezi uliopita wakati Liverpool ikicheza dhidi ya Everton baada ya kugongana na Jordan Pickford.

Mholanzi huyo sasa ana uwezekano mkubwa wa kuukosa msimu wote na hata kwenye michuano ya Euro 2020 ambayo inafanyika mwakani.

Kukosekana kwake ni pigo kubwa zaidi kwa Liverpool ambao walimtegemea kama nguzo yao tangu aliposajiliwa kwa fedha nyingi kutoka Southampton - wakati walipomaliza kusubiri kwa kipindi cha miaka 30 kutwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu England.

Van Dijk alitengeneza pasi (3,255) ambazo ni nyingi zaidi kuliko mlinzi yeyote kwenye Ligi Kuu England.

Na sasa Seedorf amekubali kwamba, pengo la Van Dijk haliweze kuzibika, lakini amekitaka kikosi hicho kuendelea kupambana.

Seedorf ameiambia Stats Perform News: "Nilihuzunika kwa kile kilichomtokea, hasa nikiwa najua morali yake na ari yake."

# VAR yamchefua Milner

**LIVERPOOL,** England

JAMES Milner amedai "anaanza kuishiwa mapenzi na mchezo wa soka" baada ya utata wa maamuzi ya VAR kuifanya Liverpool kuondoka na sare ya bao 1-1 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Brighton and Hove Albion, juzi Jumamosi.

Bao la Diogo Jota la dakika ya 60 lilionekana kama lingewapa pointi zote tatu kileleni mwa msimamo, na VAR ilikataa mabao mawili ya mapema kutoka kwa Mohamed Salah na Sadio Mane.

Pascal Gross alifunga bao kwa penalti dakika ya 93 la kusawazisha na hivyo kuwafanya 'Wekundu' hao kufikisha mchezo wa nne bila ushindi baada ya Danny Welbeck kufanyiwa madhambi eneo la hatari, hivyo kuzawadiwa penalti.

Milner, ambaye alitolewa nje baada ya kuumia misuli huku zikiwa zimesalia dakika 16 mchezo kumalizika, alionekana kuwa na ghadhabu na VAR kuwanyima ushindi na akaandika kwenye ukurasa wake wa Twitter kuelezea hali hiyo.

"Ni wazi kwamba, tunahitaji mjadala mpana kuhusu VAR," aliandika.

"Kwa uhakika siko peke yangu ninayefikiria kuanza kuishiwa mapenzi na mchezo huu kwa hali ilivyo sasa.

"VAR imepoteza kabisa ladha ya mchezo wenyewe, tunatakiwa kwa pamoja kujadiliana hili na kuangalia hatima yake kabla ya mambo hayajawa mabaya zaidi."





# PIRLO ATAKA UIMARA JUVE BILA RONALDO

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Andrea Pirlo, amesema mabingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A, lazima wajifunze kuwa bila Cristiano Ronaldo baada ya nyota huyo kuukosa mchezo wa Jumamosi dhidi ya Benevento.

Ronaldo alipumzishwa wakati Juve wakionyesha kiwango kibovu na wakalazimishwa sare ya kufungana bao 1-1 na Benevento.

Bao la Alvaro Morata la ufunguzi la dakika ya 21 lilisawazishwa na Gaetano Letizia kuelekea mapumziko.

Juve wamepitwa pointi tatu na vinara AC Milan na Pirlo alikishauri kikosi chake kuimarika wakati wanapomkosa Ronaldo ambaye amefunga mabao nane katika mechi tano za Serie A msimu huu.

"Ronaldo ni mchezaji muhimu sana, si kwetu sisi tu," alisema Pirlo akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Alikuwa kule Real Madrid na sasa Juventus.

"Aina ya wachezaji kama hawa ni wa mchezo na mabao, lakini lazima tushinde mechi bila uwapo wake au akiwapo Ronaldo. Tunatakiwa kuimarika."

Juve wameshinda mchezo mmoja tu kati ya mechi zake tisa za ugenini za Serie A.

# Conte awapa somo Inter Milan

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amewashauri wachezaji wake wa Inter Milan kujikita zaidi kwenye ubora wao badala ya kusikiliza shutuma juu yao, wakati wakiibuka na ushindi mtamu wa mabao 3-0 dhidi ya Sassuolo, Jumamosi.

Ushindi huo wa Inter, kilikuwa kipigo cha kwanza kwa Sassuolo msimu huu na sasa Nerazzurri hao wamefikisha mechi 11 bila kufungwa nyumbani kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Matokeo hayo yaliwafanya kupunguza machungu ya kuchezea kichapo cha 2-0 kutoka Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mapema wiki hii, na Conte alisifia umoja wa timu yake licha ya kupata shutuma nyingi msimu huu.

"Hongera kwa vijana kwa sababu si kazi rahisi kucheza hapa Inter," alisema akiiambia Sky Sport Italia. "Haijalishi, hatuwezi kuendelea kufikiria kuhusu shutuma kila wakati.

"Tunatakiwa kuwa vizuri, kuwa na ari, kujifikiria sisi wenyewe kufanya kazi kwa bidii. Tunahitaji kujua kwamba kuna watu ambao mara zote hawasubiri kukulaumu.

"Na ukiziangalia zaidi shutuma zinawafanya wachezaji kuwa na wakati mgumu wa kucheza kwa bidii na kuonyesha viwango vyao.

"Hali kama hiyo inatakiwa kutupa sisi morali zaidi, maana shutuma kamwe haziwezi kuisha."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




## ●●● Hakuna sababu kwa kipigo hiki, tulicheza vibaya, mimi ndiye natakiwa kulaumiwa...

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amekubali Real Madrid walionyesha kiwango kisichokubalika wakati mabingwa hao watetezi wa LaLiga walipokumbana na kipigo kingine kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania.

**Cadiz, Shakhtar Donetsk na Valencia tayari zimeifunga Madrid msimu huu, na Deportivo Alaves wakaongeza jina lao kwenye orodha ya kuwachapa miamba hao, wakati walipoibuka na ushindi wa mabao 2-1, Jumamosi.**

Mchezo huo ulionekana kuwa na malalamiko mengi kutoka kambi ya Madrid wakilalamikia maamuzi ya VAR.

Lakini kocha wa Madrid, Zidane alikuwa wazi kukubali kwamba timu yake ilistahili kichapo hicho pale kwenye dimba la Alfredo Di Stefano, ambapo miamba hao wa Hispania walipoteza mchezo wao wa tatu kwenye LaLiga msimu huu.

Walifungwa na Cadiz na baadaye Shakhtar kwenye Ligi ya Mabingwa wakiutumia Uwanja wa Alfredo Di Stefano wakati ule wa Santiago Bernabeu ukiwa unakarabatiwa.

Katika mchezo huo mabao ya Lucas Perez na Joselu ndio yaliyoipa Alaves uongozi wa 2-0 kabla ya Madrid kupata bao la kufutia machozi kutoka kwa Casemiro, huku shuti la Isco likigonga mwamba.

Kufungwa penalti ya dakika za mwanzo iliyowekwa kimiani na Perez kuliwapa wakati mgumu Madrid kusawazisha bao hilo, hasa Alaves wakionekana kucheza kwa kiwango cha juu zaidi kuliko wao.

"Wakati ukianza mchezo kama vile, kila kitu kinakuwa kigumu. Hatukuwa makini," alisema Zidane akiiambia Movistar LaLiga.

"Hakuna sababu kwa kipigo hiki. Tulicheza mchezo mbaya. Mimi ni kocha na ndiye natakiwa kulaumiwa.

"Lazima tufunge ukurasa. Jumanne tuna mchezo mwingine (dhidi ya Shakhtar). Tutaendelea kufanya kazi. Tunakwenda kubadilika kabisa."

Madrid ipo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikipitwa kwa pointi sita na Atletico Madrid na Real Sociedad.

Hicho ni kipigo cha tatu katika mechi zake tano zilizopita kwenye mashindano yote.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KUMUUZA PEPE

ARSENAL ipo tayari kumuuza winga wake wa kimataifa wa Ivory Coast, Nicolas Pepe ikiwa kutapatikana mnunuzi mzuri wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Daily Star on Sunday)***

### PIQUE IMANI KWA MESSI

MLINZI wa Barcelona raia wa Hispania, Gerard Pique mwenye umri wa miaka 33, anatumaini klabu hiyo ya Nou Camp "itazungumza vizuri" na Lionel Messi ili abaki klabuni hapo. ***(ESPN)***

### MBAPPE KIPAUMBELE MADRID

KIPAUMBELE cha Real Madrid ni kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 21, mwaka 2021 kabla ya kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland, 20, kutoka Borussia Dortmund mwaka 2022. ***(AS)***

### CITY YAJITOA KWA MARTINEZ

KLABU ya Manchester City imekuwa ikimnyatia Lautaro Martinez kwa zaidi ya mwaka, huku Barcelona na Real Madrid pia zikionyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, wa Inter Milan. ***(Sunday Mirror)***

### CHELSEA YAMWANIA MESSI

CHELSEA "inatathmini" ikiwa itamsajili nyota wa Argentina, Lionel Messi kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, ataondoka Barcelona. ***(Sunday Express)***

### ERIKSEN KUONDOKA INTER

MTENDAJI Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, amesema kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 28, ataondoka klabuni hapo Januari wakati dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa. ***(Sky Sports)***

### COUTINHO HAONDOKI BARCA

WAKALA wa Philippe Coutinho, 28, amesema mchezaji huyo hana mpango wa kuondoka Barcelona baada ya kuhusishwa na Juventus. ***(Mundo Deportivo)***

### BERARDI AWEKWA SOKONI

WAKALA wa Domenico Berardi, 26, wa Sassuolo amesema mshambuliaji huyo wa Italia thamani yake ni euro milioni 50 na hana mpango wa kulazimisha kuondoka kwa miamba hao wa Serie A. ***(Football Italia)***

### LAUTARO KUONDOKA INTER

NYOTA wa Argentina, Lautaro Martinez , 23, anataka kuondoka Inter Milan na amemweka wakala wake Jorge Mendes kusimamia utafutaji wa klabu atakayohamia. ***(Marca)***

### GOMES ATOBOA SIRI UTD

WINGA wa Uingereza, Angel Gomes, mwenye umri wa miaka 20, amesema aliondoka Manchester United 'kutafuta mwanzo mpya' baada ya kukataa ofa yao na kujiunga na Lille. ***(Independent)***

HABARI MICHEZO

## Azam hasira kwa Biashara Utd leo

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupoteza mechi mbili mfululizo za Ligi Kuu Bara, Azam FC itakuwa na nafasi ya kujiuliza na ikiwezekana kushusha hasira zake itakaposhuka katika Uwanja wa Karume mkoani Mara leo kuwavaa wenyeji wao, Biashara United.

Azam iliyokuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, imepoteza mechi mbili mfululizo zilizopita dhidi ya KMC FC na Yanga, zote ikilala kwa bao 1-0, hatua iliisosababisha kutimuliwa kwa Kocha wao Mkuu, Mromania Aristica Cioaba.

Kwa sasa timu hiyo ipo chini ya Kocha Msaidizi, Vivier Bahati, ambaye ataiongoza kwenye mchezo huo na kisha dhidi ya Gwambina FC. Akizungumza mchezo huo wa leo, Ofisa Habari wa Azam FC, Zakaria Thabit 'Zaka Zakazi', alisema maandalizi yote ya mechi hiyo yapo vizuri na kocha ana matumaini makubwa ya kuvuna alama tatu.

"Tupo tayari kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Biashara United ni matumaini yetu kocha ataiongoza timu kufanya vizuri na kupata pointi tatu ili turejee kwenye ubora wetu," alisema wakati huu wakiwa nafasi ya pili na pointi zao 25, sita nyuma ya Yanga iliyopo kileleni lakini ikiwa na mechi moja mbele.

## Adam aukana uchoyo Yanga

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa JKT Tanzania aliyeibuka kuwa hatari kwa siku za karibuni, Adam Adam, amekanusha kuwa mchoyo kwenye mechi dhidi ya Yanga katika baadhi ya matukio kwa kueleza kwamba kwenye soka mambo hayo hutokea.

Akizungumza baada ya timu yake kupokea kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Yanga, Adam alisema yeye si mchoyo na kwamba kilichotokea ni hali ya mpira na huwa inajitokeza, pale mchezaji anapoona anaweza kufunga bao.

Baadhi ya mashabiki walimtuhumu kuwa kuna nafasi kama mbili au tatu alikuwa na uwezo wa kutengenezea wenzake ili wasawazishe bao hilo, lakini alipiga mashuti ambayo yalipaa juu ya lango.

"Ni kweli hiyo imetokea, lakini siyo kwa sababu ya uchoyo, kwenye soka mambo kama hayo yapo kwa sababu ningepiga na kufunga haya yote yasingesemwa, lakini kwa kuwa nimekosa, ndiyo inaonekana hivyo," alisema mchezaji huyo ambaye kwa sasa anaichezea pia timu ya Taifa, Taifa Stars.

Alisema hali ya kukosa matokeo kwenye kikosi chao haiwakatishi tamaa na kwamba watapambana kwa hali yoyote ili waiweke timu yao nafasi nzuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mpaka sasa Adam si tu kwamba ndiye mfungaji anayeongoza kwa kupachika mabao kwenye kikosi cha JKT Tanzania, lakini anakamata nafasi ya pili nyuma ya John Bocco wa Simba mwenye mabao saba, huku yeye akiwa amecheka na nyavu mara sita.

# WASUDAN WA NAMUNGO FC WATAKA MARUDIANO NCHINI

**Na Saada Akida**

WAPINZANIA wa Namungo FC kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Al Rabita FC ya Sudan Kusini, wamewaangukia wawakilishi hao wa Tanzania wakitaka mechi yao ya marudiano ichezwe hapa nchini, imefahamika.

**Katika mechi ya awali iliyopigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, Namungo iliibuka na ushindi wa mabao 3-0, shukrani kwa Steven Sey aliyetupia mawili na mtokea benchi Shiza Kichuya aliyehitimisha ushindi huo.**

Nipashe lilipata taarifa hizo juzi za Al Rabita kutaka mechi hiyo ya marudiano ichezwe tena hapa nchini kutokana na uwanja wao huko Sudan Kusini kutokuwa na vigezo vinavyohitajika na CAF, na lilipomtafuta Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu, alikiri klabu hiyo kupokea maombi hayo kutoka kwa wapinzani wao.

"Wametueleza sababu ya kutaka kuendelea kutumia moja ya viwanja vyetu hapa nchini kwa ajili ya mechi ya marudiano, hivyo uongozi wa Namungo tumewakubalia, sasa tunasubiri taarifa kutoka ngazi ya juu ni uwanja gani ambao tutatumia," alisema Zidadu.

Akizungumzia ushindi huo wa juzi, Kocha Mkuu wa Namungo, Hemed Morocco, alisema kwa upande wake ni matokeo mazuri kwa sasa kwa kuwa hakuwaona wapinzani wao zaidi ya walipokutaka juzi katika mechi hiyo ya awali.

"Nimeona ubora wao na madhaifu yao, nina imani mechi yetu ijayo ya marudiano tutafanya vizuri zaidi na kuvuka hatua hii, kwa sababu tunaenda kufanyia kazi kasoro zetu," alisema Morocco ambaye hiyo ni mechi ya pili kuiongoza Namungo tangu atwae mikoba hiyo kutoka kwa Mnyarwanda Thierry Hitimana aliyetimuliwa kutokana na matokeo mabaya.

Morocco ambaye mchezo wa kwanza kuiongoza Namungo ulikuwa wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga kwenye Ligi Kuu Bara, alisema anaenda kujipanga kwa ajili ya mchezo huo na huenda mechi ya marudiano na kama wakiruhusiwa kucheza hapa nchini ana imani kubwa ya kufanya vizuri zaidi.

Alisema imani hiyo inatokana na ukweli kwamba watakuwa tena nyumbani katika viwanja ambavyo wachezaji wake wamevizoea.

Hii ni mara ya kwanza kwa Namungo kushiriki michuano ya kimataifa baada ya kupanda Ligi Kuu Bara msimu wa 2019/20.

KATUSUA...




Mshindi wa Bonasi ya Jackpot, Andrew Maganga, mkazi wa Ukonga jijini Dar es Salaam akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 5.6 aliyokabidhiwa mwishoni mwa wiki, baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa. Kila wiki SportPesa huwazawadia bonasi washindi wanaobashiri kwa usahihi mechi 10-12 kwenye Jackpot hiyo. **PICHA: SPORTPESA**

# *Kocha Mlandege atoa sababu kipigo CAF*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HUKU akitoa sababu ya kipigo mithili ya 'mbwa mwizi' juzi baada ya timu yake kukubali kulala kwa mabao 5-0 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Mlandege FC, Abdulmutik Haji, amesema kupoteza katika uwanja wao wa nyumbani haimaanishi timu hiyo imekata tamaa ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

Akizungumza baada ya kumalizika mechi hiyo iliyopigwa katika Uwanja wa Amaan visiwani hapa, na wapinzani wao, CS Sfaxien kutoka Tunisia kuishindilia kipigo hicho cha mbwa mwizi, alisema mpira ni mchezo wa makosa na ana imani pengine katika mechi ya marudiano atapata nafasi ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

Alisema katika mchezo wa soka lolote linaweza kutokea na kwamba kikubwa ni kuwajenga wachezaji kisaikolojia ili kwenda kupambana kupata matokeo na hatimaye kusonga mbele kwenye michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

"Sijakata tamaa ya kusonga mbele, inawezekana katika mechi ya marudiano tukapata nafasi nzuri na tukafanikiwa kuvuka, hivyo kikubwa wachezaji tuwajenge kisaikolojia ili wapate nguvu ya kupambana," alisema.

Aidha, akizungumzia mchezo huo, alisema kosa kubwa lililowasababishia kufungwa mabao mengi ni wachezaji kutokuwa na uzoefu wa kucheza mechi za kimataifa, hivyo ilikuwa vigumu kuwa wepesi kiakili kupangua mbinu za wapinzani wao uwanjani.

Alisema licha ya ugeni wa mechi za kimataifa, lakini asilimia kubwa ya wachezaji wao ni wafupi wa kimo ikilinganishwa na wapinzani wao ambao wengi ni warefu na wenye uzoefu kisoka.

Hata hivyo, alisema wachezaji walijitahidi kupambana na hata ukiangalia mabao yaliyofungwa karibuni yote yametokana na mipira 'iliyokufa' ya [adhabu ndogo] tena kwa kichwa kutokana na urefu wao.

Mlandege itakuwa na kibarua cha kuhakikisha inashinda kuanzia mabao 6-0, ili kusonga mbele wakati timu hizo zitakaporudiana nchini Tunisia Desemba 6, mwaka huu.

# Michezo

Jumatatu Novemba 30, 2020

Nipashe




Zidane alalamikia kiwango Madrid UKURASA 22




Bondia wa zamani wa uzito wa juu, Mike Tyson (kushoto), akimsukumia konde Roy Jones Jr katika pambano la raundi nane la kukumbushia enzi zao lililopigwa jana asubuhi katika Ukumbi wa Staples Center jijini Los Angeles, Marekani, ambalo lilimalizika kwa majaji kujiridhisha kuwa wawili hao wametoshana nguvu, droo. Hata hivyo, mashabiki wa masumbwi waliwakosoa majaji, wakidai Tyson aliyekuwa anapigana baada ya miaka 15 alistahili ushindi. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yanguruma Nigeria

## ●●● Muziki wa Chama, Miquissone waizima Plateau, mechi ikichezwa dakika 98 huku...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Tanzania Bara Simba, jana walinguruma kwenye Uwanja wa New Jos mjini Jos, Nigeria baada ya kuwachapa mabingwa wa nchi hiyo, Plateau United kwa bao 1-0 kwenye mechi ya raundi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Alikuwa ni Mzambia Clatous Chama aliyepeleka furaha kwa wanachama, mashabiki wa timu hiyo na Watanzania kwa ujumla, alipofunga bao pekee dakika ya 53.**

Chama alifunga bao hilo baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Luis Miquissone alipowalamba chenga mabeki wa Plateau na kummegea mfungaji aliyeujaza wavuni na kumuacha kipa Abubakar Adam akiwa hajui la kufanya.

Kwa matokeo hayo, Simba italazimika kushinda au kupata sare yoyote ile nyumbani nchini Tanzania kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam timu hizo zitaporudiana Jumamosi wiki hii, ili iweze kusonga mbele na kuingia raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

Hii ni mara ya kwanza kwa Simba kwenye historia yake, si kuifunga timu ya Nigeria nyumbani kwao tu bali hata kupata bao dhidi ya timu za nchi hiyo zikiwa katika ardhi yao.

Timu hiyo ilishacheza na timu za Racca Rovers na Enyimba bila kupata hata bao ugenini, huku ikipata vichapo vya uhakika na kutwa nje ya michuano hiyo.

Dalili za Simba kushinda mechi hiyo zilianza mapema tu dakika ya 11, baada ya nahodha wao, John Bocco alipoingia ndani ya eneo la hatari na kuachia shuti lililotoka nje.

Hata hivyo, kibao kiligeuka baada ya wenyeji kuja juu dakika mbili baadaye na kufanya shambulizi kali lililozaa kona mbili za hatari, ya kwanza ikipanguliwa na kipa Aishi Manula kutokana na mpira wa kichwa uliopigwa na Sunday Adetunji na kuwa kona nyingine ambayo nayo ilipigwa tena na Gabriel Wassa, lakini kichwa kilichopigwa na Saed Jibril kiligonga mwamba na kuokolewa na mabeki wa Simba waliokuwa wakiongozwa na Paschal Wawa.

Dakika ya 42, wachezaji Hassan Dilunga na Jonas Mkude walikosa mabao ya wazi, baada ya kutokea piga nikupige kwenye lango la Plateau.

Kipindi cha pili Simba ilifanya mabadiliko kwa kumtoa Joash Onyango na kumuingia Mzamiru Yassin ambaye aliongeza uhai na kuanza kufanya mashambulizi mfululizo, hadi bao pekee lilipopatikana.

Baada ya bao hilo, Simba ilionekana kucheza kwa nidhamu kubwa ikifanya mashambulizi ya kushtukiza, huku Plateau United ikifanya mashambulizi makali kupitia kwa Andrew Ike, Issa Ndala na wengineo.

Simba nusura ipate penalti dakika za mwisho wa mchezo, baada ya Banard Morrison aliyeingia kuchukua nafasi ya Hassan Dilunga, alipoangushwa ndani ya eneo la hatari, lakini wakati mwamuzi akiamuru itengwe penalti, mwamuzi msaidizi alikataa.

Hata hivyo, licha ya mechi kutokuwa na matukio mengi ya kupoteza muda, ilichezwa kwa dakika 98. Simba iliwakilishwa na Manula, Shomari Kapombe, Mohamed Hussein, Joash Onyango/ Mzamiru Yassin, Pascal Wawa, Jonas Mkude, Hassan Dilunga/Bernard Morrison, Erasto Nyoni, John Bocco, Clatous Chama/Ibrahim Ame na Luis Miquissone.

Endapo Simba itapata matokeo ya jumla katika mechi ya marudiano, itakutana na Costa do Sol ya Msumbiji ama FC Platinum ya Zimbabwe ambayo nayo imetanguliza mguu mmoja mbele baada ya mchezo wa kwanza kushinda kwa mabao 2-1 ugenini.

# Kaze na uamuzi mgumu Yanga

**Na Saada Akida**

HUKU akisifu uwezo unaoendelea kuonyeshwa na winga wake, Deus Kaseka, Kocha Mkuu wa Yanga, Mrundi Cedric Kaze, ameweka wazi kamwe hataivumilia safu yake ya ushambuliaji kutokana na ukame wa mabao unaoendelea kuiandama timu hiyo, wakati huu dirisha dogo la usajili likikaribia kufunguliwa hapo Desemba 15, mwaka huu.

Kaseke ameipa Yanga ushindi katika mechi mbili mfululizo dhidi ya Azam FC na JKT Tanzania wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 katika michezo hiyo.

Safu ya ushambuliaji Yanga ambayo inaongozwa na Mghana Michael Sarpong, Mburkina Faso Yacouba Songne na Ditram Nchimbi, imecheka na nyavu mara 15 tu katika michezo 13 ilizocheza huku safu yao ya ulinzi ikionekana kuwa imara zaidi kwa kuruhusu mabao manne tu na ikiwa timu pekee ambayo haijapoteza mechi ya Ligi Kuu Bara hadi sasa msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana baada ya mechi dhidi ya JKT Tanzania iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Kaze alisema tangu atue nchini na kuanza kuinoa timu hiyo kwenye mechi nane hadi sasa, hajawahi kuwa na chaguo moja la mshambuliaji.

Alisema amekuwa akiwachezesha kwa mzunguko washambuliaji wake kwa kumpa nafasi Sarpong, Nchimbi mara nyingine Yacouba, lakini wameshindwa kuzitumia nafasi wanazozipata na hivyo timu kuishia kupata ushindi finyu wa bao 1-0 huku yakifungwa na mawinga au viungo.

"Katika mechi tulizocheza tumekuwa tukitengeneza nafasi nyingi tunashindwa kuzitumia, ukiangalia leo (juzi), tumekosa nafasi nyingi, sitachoka kuwapa mbinu ila ikishindikana inabidi tukae chini na kuangalia uwezekano wa kutafuta mtu ambaye atafanya kazi hiyo vizuri.

"Mfano mzuri leo (juzi) tulivyocheza hasa kipindi cha pili, tumecheza kwa presha kubwa ya kujilinda ili wapinzani wasisawazishe, suala hili linatakiwa kufanyiwa kazi haraka," alisema.

Kuhusu nyota Kaseke, Kaze alisema: "Kaseke ni mchezaji ambaye amekuwa akifanya jambo sahihi na wakati sahihi anapokuwa uwanjani, na kuipa timu matokeo mazuri katika michezo miwili mfululizo."


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >